# Tunataka Kumwona Yesu

Grass Valley, California, Amerika
Julai 04, 1962

1 Asante, ndugu. Mnaweza kuketi. Hakika ni tunu kuwa haMa katika Grass Valley jioni hii, ili kumwakilisha Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo; ili kuwaombe watoto wa Mungu walio wagonjwa, mgonjwa wa Daktari; na ili kufurahia huu ushirika Mamoja, kwa hizi siku tano tulizoahidiwa.

Naleta salamu kutoka kwa wasafiri wengine wote katika sehemu mbalimbali za ulimwengu kwa wale ambao niliwafikia. Na kwa kutumaini ... Na maelfu mengi ya watu wanaomba kwa ajili ya mafanikio ya huu mkutano hapa, nyakati hizi za jioni. Nina hakika, Mamoja na maombi ya hao wengine, na sisi wenyewe, kwamba Mungu atakutana na sisi na kutubariki.

Na sisi hatuji sasa ili kuliwakilisha kanisa fulani lolote, au hatuji ili kujiita sisi wenyewe "waponyaji." Sisi tunakuja, tukiwa tunamwakilisha Kristo. Na tunakuja, pia, siyo kuponya wagonjwa, bali ili kuomba kwa ajili ya wagonjwa, na kufanya kile ambacho tunaweza kusaidia ili kufanya maisha yawe marahisi zaidi kidogo kwa ajili ya kila mmoja. Na nina hakika kuwa mtakuwa baraka kwetu. Na tunatumaini kuwa sisi tutakuwa baraka kwenu.

2 Na sasa nilikuwa nikiwazia tu, kwa kuwa tumekuwa kule California hii safari ya mwisho, kwamba watu wangefika nyumbani mapema. Sasa, kule nyumbani, na mbalimbali, sehemu nyingi za nchi, unakuta watu mbalimbali. Baadhi yao, wao wanapenda tu kukusikia ukihubiri; mimi sijali hata kama wewe huombi kwa ajili ya wagonjwa, kuwaweka tu wao kwa kama saa nne au tano, ukihubiri, hilo-hilo huwatosheleza tu wao. Lakini hapa, hakika linaumiza; wao wanaonekana kama kwamba, "Mahubiri mafupi tu, na kuombea wagonjwa, na hebu turudi nyumbani kwa haraka kwa sababu inanipasa nirudi tena." Na kila kitu kinaonekana kama kwamba katika uharaka hapa. Sote tunakwenda wapi? "Haraka, haraka, haraka, haraka, haraka!" Huenda, Bwana akipenda, nataka kuhubiri niwapo hapa, Kuondoa Hasira. Nafikiri hilo ndilo-hilo ndilo tunalopaswa kufanya, namna ya kuachia tu.

3 Nilipata tu ajali, wiki chache zilizopita. Napenda kupiga lengo risasi, kuwinda. Nilikuwa nimepewa tu bunduki, ambayo iliyokuwa imetengenezewa mtutu upya na Kampuni ya Weartherby chini hapa. Na nikainua kile kitu juu, ili kupiga risasi, na ikalipuka usoni mwangu. Na ikalipua mtutu ule kama yadi hamsini, mbele yangu, na tako kama umbali ule ule nyuma yangu, na kulipua vichaka na kila kitu pale, pale kile kitu kilipokwenda. Na kwa neema ya Mungu tu haikunilipua mimi hivyo hivyo, kwa sababu ilikuwa karibu kiasi hicho kwenye jicho langu ilipopiga, nilipoiweka, darubini ikiwa juu, nikipiga.

Na ninalo wazo dogo kutokana na hilo. Unaona, ile-ile bunduki kwa kweli haikuwa bunduki ya Weatherby. Hiyo ilikuwa imetengenezewa mtutu kutokana na bunduki ya Weatherby. Ilikuwa ni aina ya Winchester sabini, kwenu ninyi jamaa mnaowinda. Nayo nilikuwa nimepewa na ndugu mwema wa California aliyeitwa Art Wilson. Yeye alimpa mwanangu, Billy Paul, aina ya Roberts mia mbili hamsini na saba. Na hivyo wao ... Billy ni wa mkono wa kushoto, na kamwe hakuwahi kuitumia hiyo, hivyo yeye akasema, "Baba, nitakupa tu hiyo."

4 Vema, mimi-mimi siku zote nilitaka bunduki aina ya Weatherby, lakini nilijiskia kutokuweza kununua moja. Na basi kama baadhi ya marafiki zangu wangeninunulia moja, ningeliwataka wao kufanya hilo, kwa sababu hizo ni bunduki za ghali. Na kama ambavyo nimekuwa nikisema siku zote, "Ninao marafiki wamishenari ambao hawana viatu miguuni mwao na mimi-mimi siwezi kumwacha mtu fulani alipe kiasi hicho kwa ajili ya bunduki, ya mimi kuwindia au kupigia risasi, wakati ninao marafiki ambao hawana hata viatu." Hivyo, singeweza tu kufanya hilo.

Lakini rafiki yangu akasema, "Naweza kuchukua ile aina ya namba sabini na kutengeneza bunduki ya Weatherby kutokana na hiyo. Weatherby hufanya hilo kule, na kuitolea dhamana." Mimi nikasema ... Akasema hiyo haitanigharimu, kama 'dola kumi, kumi na mbili" tu.

Na mimi nikasema, "Endelea."

Hivyo yeye akaitoa, akaipeleka kwenye kampuni nao wakaitengenezea mtutu. Kwanza, ililipuka pale pale. Hivyo hiyo haikuwa, siyo lazima iwe...Kitu fulani kilicho na shinikizo mahali fulani.

5 Sasa somo langu juu ya hilo ni hili. Unaona, hiyo ilikuwa na shinikizo mno. Unaona? Hatuhitaji shinikizo kupita kiasi, hilo-hilo litalipuka.

Na kitu kingine, ningelipenda kusema hili, huenda hilo likawa na maana ndogo ya mafundisho ndani. Unaona, kama hiyo bunduki ingekuwa imeanzia kwenye chungu, chungu cha Weatherby, ingelilipuka. Lakini, unaona, hiyo ilikuwa kitu fulani kingine kilichobadilishwa sehemu, na hiyo ndiyo sababu hiyo haikuweza kuhimili shinikizo.

Na mimi naamini katika dini ambayo hatuiwekei viraka. Sisi tunakufa na kuzaliwa mara ya pili, na ndiMo tunakuwa Mkristo ambaye anaweza kustahimili mashinikizo yote ambayo Roho Mtakatifu anayotaka kuyatupa. Hivyo mimi-mimi nafikiri inatupasa kurejea pale mwanzo, siyo tu kujaribu tu kufanya kitu fulani kutokana na kitu fulani ambacho sicho. Tunayo dini ya kisaikolojia mno leo hii, badala ya uzoefu halisi uliozaliwa upya na Mungu. Na hivyo mahali fulani njiani kitu fulani kidogo kitakuja Male, kitasababisha kuvuja kidogo, na kurudisha shinikizo nyuma, na utajikuta mwenyewe umelipuka. Hivyo sisi tunaamini katika kufa kwa kweli wewe mwenyewe na mawazo yako yote na kila kitu kingine, kufa tu moja kwa moja na kumruhusu Roho Mtakatifu akuunde upya. Wewe-wewe unakuwa Mkristo tu aliyezaliwa mara ya pili, hicho ndicho wewe ulicho, kuwa na uzoefu na Mungu kuwa wewe unajua umekwishakupita kutoka mautini kuingia Uzimani. Na hicho ndicho sisi tunachoamini.

6 Sisi tunaamini Biblia, na tunaamini kuwa Hicho ndicho Kitabu cha Mungu. Sisi, tunadumu tu moja kwa moja na Biblia. Sasa, , mimi naamini kuwa Mungu anaweza kufanya mambo ambayo Yeye hayajaandikwa katika Biblia. Sasa, Yeye ni Mungu, Yeye anaweza kufanya chochote Yeye anachotaka. Lakini kama mimi naweza kumwona tu Yeye, katika wakati wa maisha yangu, akitenda kile Yeye alichoahidi, basi mimi najua hilo ni sahihi, unaona, maadam hilo liko katika Biblia.

Sasa, katika Agano la Kale, kama ambavyo ndugu wanaohudumu wanajua, kuwa katika ule-ule ukuhani wa Kilawi, wao walikuwa na namna ya kujua kama nabii alikuwa anasema ukweli, au ndoto ya mwotaji ilikuwa sahihi. Wao walikuwa na kile kilichoitwa Urimu na Thumimu. Sasa, hilo limepingwa lilivyokuwa. Lakini zaidi, maana kuu zaidi na iliyo ya kimaadili zaidi ambayo mimi ninaweza kuona, na kwa njia iliyofaa vema, ilikuwa, wao walichukua dirii ya kifuani iliyovaliwa na Haruni; ambayo iliwakilisha makabilia kumi na mawili kwa mawe ya kuzaliwa ya yale makabila, na hiyo ilining'inia hekaluni, juu ya nguzo. Na ndipo nabii alipotabiri, na halafu wao waliweza kujua kama hiyo ilikuwa Kweli, au hapana; sasa, kama hiyo mikusanyiko ya mianga ilimulika Male, ikifanya ya Kiungu. Mungu ni wa Kiungu, kwa sababu Yeye ni Mungu, Roho. Na kama hiyo Nuru ya Kiungu iliwakilishwa pale, kama upinde wa mvua ukimulika kutoka kwenye hili, basi neno, nabii alikuwa sahihi. Hivyo ndivyo yeye alivyotambulika, au mwota ndoto alikuwa sahihi. Lakini kama hiyo haikutoa nuru juu ya Urimu na Thumimu, basi haidhuru hilo lilikuwa linaonekana kamilifu iliyoje, wao hawakulipokea hilo, kwa sababu hilo halikutoa nuru juu ya Urimu na Thumimu.

7 Sasa, ukuhani wa Kilawi ulikwisha Menye kifo cha Bwana Yesu. Sasa tunaishi katika Ukuhani wa Melkizedeki, Kristo. Sasa sisi siyo kwamba hatuna Urimu na Thumimu. Huo ni Huu sasa, Biblia. Unaona, ni lazima tudumu na Andiko (siyo kuweka fasiri zetu kwenye Hilo) jinsi tu Hilo lilivyoandikwa. Sasa, mimi naamini kuwa-kuwa Mungu atahukumu ulimwengu siku fulani kwa njia ya Yesu Kristo. Mimi naamini hilo. Mimi naamini kuwa kutakuweko na kiwango fulani Yeye ambacho angehukumu nacho, kwa sababu kuna kuwakilishwa mno kwa Kristo, na mengi mno.

8 Sasa, asili yangu, M-Irish, hivyo watu wangu kabla yangu walikuwa Katoliki. Mimi nilipokuwa mvulana mdogo; labda mmesoma habari ya maisha yangu, wanayo hiyo hapa katika vitabu, na kadhalika. Nilikwenda chini kule kwenye kanisa la Ki-Irish na kusikia kile alichosema kasisi. NdiMo nikaenda kule kwenye kanisa la Lutherani, nikasikia kile yeye alichosema, mchungaji wa Lutherani. Na kumekuweko Baptisti ndogo nyuma mahali fulani katika kizazi chetu, hivyo wao ... Nikaenda kule kwenye kanisa la Baptisti. Nilikwenda kwenye makanisa mbalimbali. Vema, wao, kila moja, ni tofauti na jingine. Sasa, kila moja lilitaka kusema kuwa hilo kanisa lilikuwa sahihi kabisa.

Hivyo, sasa, wote hawawezi kuwa sahihi, inapasa kuwepo na kitu fulani cha makosa

mahali fulani. Na naona sasa, kuna madhehebu mbalimbali kama mia tisa na kitu, hivyo nafikiri kuna kitu fulani cha makosa mahali fulani. Bila shaka, kama hili, wote waliingia ndani kwa njia ya hili kanisa ...

9 Sasa tuliambiwa, kama Wakatoliki, kuwa-kuwa-kuwa "Mungu yuko katika kanisa Lake. Na pale ndipo Mungu alipo, katika Kanisa Lake." Hivyo basi kama Mungu yuko katika kanisa Lake, ni lipi la hayo ni kanisa Lake? Kila moja ya hayo linasema ni "lile kanisa." Hivyo nilijua kitu kimoja ... Sasa hilo ndilo tu kasisi alilosema, "Mungu yuko katika kanisa Lake."

Lakini Biblia ilisema, "Mungu yuko katika Neno Lake." Na Yeye alisema kwamba, "Yeyote atakayeongeza lolote kwenye Hili, au kuondoa lolote kwenye Hilo, kitu hicho hicho kitaondolewa kutoka kwenye Kitabu cha Uzima, kwa ajili yake." Hivyo mimi naamini kwa moyo wangu wote kwamba Hili Neno ni Mungu katika umbo la maandishi. Sasa, kwa nini mimi ninasema hilo ni kwa sababu kwamba hakuna mtu aliye bora kuliko neno lake, yeye siyo zaidi ya neno lake. Kama wewe huwezi kulichukua neno langu kwa chochote, basi huna shughuli na mimi, unaona, kwa sababu huwezi kuniamini mimi. Na ni kitu kile kile, inaniMasa kuamini kwamba Hili ni Neno la Mungu, na naamini.

10 Sasa Biblia ilisema, katika Mtakatifu Yohana, ile sura ya 1, "Hapo mwanzo kulikuweko Neno, na Neno lilikuwa pamoja na Mungu, na Neno alikuwa ndiye Mungu. Na huyo Neno alifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu," basi Huyo alikuwa Kristo, na Kristo ni Neno. Basi kama Yeye anahukumu ulimwengu kwa njia ya Kristo, itapasa iwe kwa njia ya Neno. Unaona? Hivyo, hivyo ndivyo tunavyoamini Hilo, na katika kufundisha kwetu.

Sasa tutakuwa tu na kwa kifupi, kwa haraka tunapotoka nje...Wa kwao ni upi, katika nyakati halisi, ndugu, wa kutoka nje hapa, kama saa nane au kitu fulani kama hicho? Loo? Saa nane? Wao walikuwa wanacheka, hivyo nadhani kama saa tatu au tatu na nusu, kitu kama hicho, ni kama wakati wa kutoka nje. Hiyo itakuwa ndani ya kama dakika thelathini na tano.

11 Jioni hii, mimi nikiwa mgeni miongoni mwenu, bado mimi sijisikii kwamba ni mgeni. Najisikia mimi ni ndugu yenu. Na sasa nataka ninyi mfuate kile ninachosema katika Andiko. NdiMo Ujumbe unaelekea utakuwa tofauti kabisa kuliko kile ninyi mlichokuwa mnakitarajia, lakini upitie kwa kuuthibitisha na Andiko. Utaendana moja kwa moja kwenye mstari ule ule mliousikia. Nitasoma tu Hilo kutoka kwenye Andiko, na ndipo bila kujaribu kuelezea Hilo, niliache tu Hilo lijieleze Lenyewe.

Kama kuuza bidhaa. Kama unayo bidhaa ya kuuza, kama ni nzuri, itajiuza yenyewe. Huna haja ya kutangaza mno kuhusu hiyo. Ninayo hayo mambo ya matangazo mengi mno, kwamba na-natembea huko na huko, unaona ... kila mtu ni "mtu wa wakati," na "huu ni ujumbe," na hilo lote, hadi najiuliza yeye ni nani. Ee, mimi naamini Kristo ndiye Mtu wa wakati, na siku zote amekuwa hivyo. Na ufahari mwingi na mambo haipasi kuwekwa juu yake.

Nilikuwa na hilo la kutosha wakati mmoja. Kweni ninyi akina dada ... Mimi-mimi ninaye mke wangu, yeye yupo pamoja nasi, na kwa kweli nampenda yeye na watoto wangu. Na hivyo siku zote nataka kumsaidia, na mimi sijui sana katika kusaidia. Na mimi nilikuwa ... Najua yeye anayo mengi mno ya kufanya, na watoto, kuandaa kila kitu kuwa tayari, kwenda kulala usiku mimi niwapo nyumbani. Mimi nilifikiri ningemsaidia yeye kuosha vyombo, mimi ninachukia vibaya tu kufanya hilo kama ninyi. Na nikawaza, "Vema!"

12 Na mama alikuwa amezoea kunisimamisha juu ya sanduku dogo la kuoshea vyombo nilipokuwa mvulana mdogo, na mimi nikawaza, "Kama nikioa, nakwenda kuondokana na hiyo tabia sasa hivi."

Lakini ndiyo hii hapa, nampenda mke wangu jinsi nilivyompenda mama yangu, kama tu mke, na mama yangu. Ndipo nikawaza, "Vema, nitamsaidia yeye kama nitaweza."

Na niliona jambo fulani kwenye kipindi wakati mmoja, kipindi cha televisheni, pale nilipokuwa nikisubiri ndani-eropleni ili kutoka nje, nao walikuwa na televisheni ikiwa imekaa nje pale na sehemu ya mbele iliyo kubwa, kioo kikubwa ndani yake, nayo ikasema, "Tumia sabuni fulani, hakuna kuosha, hakuna kusuuza, hakuna kupangusa, hakuna chochote. Weka tu hiyo ndani ya maji, tumbukiza hicho chini, kitoe, ni hilo tu

unalopaswa kufanya."

Mimi nikawaza, "Loo! Mke wangu atanipenda hasa kuanzia sasa na kuendelea, kwa sababu ninakwenda kumwonyesha yeye jinsi ya kufanya vyombo." Hivyo, nikachukua pakiti moja ya hiyo, siku iliyofuata nilipofika nyumbani. Nikachukua pakiti moja kabla ya kwenda nyumbani, nikaiweka chini ya koti langu, na kuingia ndani.

13 Asubuhi iliyofuata, mimi nikasema, "Usijali, mpenzi. Mimi niko haMa haMa ili kuosha vyombo kwa ajili yako. Ni hilo tu linalokupasa kufanya. Sasa utoke tu moja kwa moja nje pale na uchukue ufagio na kuanza. Kabla mimi sijaenda ofisini au kuanza kupiga simu zangu, nitakuwa nimemaliza kuosha vyombo katika muda mfupi."

Hivyo nikachukua hiki kitu na kusoma juu yake, unajua, "Weka vijiko viwili vya chakula." Na mimi nikawaza, "Jamani, nitafanya kazi hasa kutokana na hiyo." Nikamwagia kama nusu ya kiboksi ndani mle, nikaikoroga namna hiyo; nikachukua vyombo vyote na kuviweka chini ndani namna ile, mapovu yakatoka kama kimo hicho. Nikawaza, "Jamani, kwa dakika chache tu sasa, na la kufanya tu ni kuviondoa na kuviweka mezani tena." Watoto walikuwa wamekula mayai kwa ajili ya kifungua kinywa; nikavitoa nje, kulikuweko na mayai kama vile mwanzo.

Hivyo nikasema, "Ninapoona kitu chochote kinachotangazwa kwa hali ya juu, napita tu kando yake tangu wakati huo na kuendelea, hakinisumbui, kwa sababu mimi najua hilo halikufanya kazi kwenye lile."

14 Na hivyo mara nyingine nafikiri kwamba kama tukizungumza tu juu ya Yesu na kuachia watu waone Yeye ni nani, na kile-kile Yeye alicho, na naamini kwamba ninii…Yeye, atafanya hayo mengine ya hilo. Yeye atajileta Mwenyewe, kwa sababu "Wote Baba alionipa Mimi watakuja Kwangu, kwa vyovyote." Unaona, hilo ndilo Yesu alilosema. "Na hakuna mtu awezaye kuja asipoitwa na Baba Yangu." Hivyo kitu pekee tunachofanya ni kupanda tu mbegu, na kuiacha iende.

Sasa, natumaini kuwa mtakwenda kwenye simu na kupigia watu.

Na jambo kuu hapa siyo kuombea wagonjwa sasa, hilo ni mojawapo ya mambo madogo, lakini jambo kuu ni kumpata kila mwenye dhambi tunayeweza ili amjue Bwana Yesu kama Mwokozi wake. Hilo ndilo kuu. La pili, ni kumfanya kila mtu aliyempokea Kristo kama Mwokozi wao, na ambaye bado hajajazwa kwa Roho Mtakatifu, kwa wao kujazwa kwa Roho Mtakatifu. Na hilo ndilo la pili kwako. Jambo la tatu, ni kuombea wagonjwa ambao tunaweza kuwaombea. Na, kupitia hilo, tunatumaini Mungu atatupa sisi wakati mkuu katika huu mkutano. Na nafikiri ni kila jioni na ndipo Jumapili alasiri, nafikiri, ni-ni sahihi.

15 Nataka niwashukuru ndugu zangu hapa, wahudumu, kwa kunialika hapa. Na namshukuru Mungu kwa uongozi wa kuja hapa. Sasa, meneja hapa, Bwana Borders, tulikuwa na kitabu kilichojaa mialiko ulimwenguni kote, lakini kwa namna fulani Kitu Fulani kilinena nami juu ya Grass Valley.

Na mara moja, rafiki yangu, familia ya Arganbright chini hapa Los Angeles, aliniita mimi na kusema, "Kama hujapanga utaratibu wa safari yako kabisa ya kwenda, natamani ungesimama katika Grass Valley."

Mimi nilimpigia simu meneja, nikampata kwenye simu, nikasema,

"Umekwishakupitia pale?"

"Hapana."

Mimi nikasema, "Pitia pale." Na sisi ndio tuko hapa.

Sasa kile Bwana anachokwenda kufanya, mimi sijui. Huenda pakawepo na mtu mmoja hapa Yeye yuko kwa ajili yake, anakuja kwa ajili yake. Natumaini ni jumuia yote ambayo Yeye anakuja kuiokoa.

Sasa, juu ya hili, hebu tuinamishe vichwa vyetu na tunene na Mwanzilishi kabla ya kusoma Neno Lake.

16 Baba yetu wa Mbinguni, ni tunu kuu hasa tuliyo nayo, kwa kusimama katika Uwepo Wako, katika hii saa ya kufunga ya historia ya huu ulimwengu, na kukuita Wewe "Baba," na tukijua kuwa tunakukaribia Wewe kwa Njia inayotosha kabisa, kwa uhakika wa baraka ambao Yesu, Mwanao, alisema, "Kama mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, Mimi nitalifanya hilo, tutajaliwa hilo." Basi sisi tunajua, Baba, kama tukiomba

katika Jina la Bwana Yesu, kwamba maombi yetu tutayapewa. Sasa tusingetaka kuomba chochote kinyume na mapenzi Yako. Lakini tunaamini uongozi Wako hapa, na kujaza watu kwa Roho Mtakatifu, na kujiMatia utukufu Wewe Mwenyewe. Na tuko sisi hapa ili kufanya kila kitu ambacho Wewe utatuongoza sisi kufanya. Hivyo naomba, Baba, kwamba utalifunua Neno Lako kwetu, na Wewe mapenzi Yako, kwa Neno Lako, kwamba tuweze kujua maMenzi Yako ni nini kuhusiana na Neno Lako. Tubariki sisi sote kwa Mamoja sasa. Tusamehe dhambi zetu.

17 Na jioni hii, tunapotulia katika hili jengo, tunaomba kwamba Wewe utabariki hili jengo. Mungu, labda ni uwanja, lakini huo sasa unawekwa wakfu kwa ajili ya ibada ya Mungu Mwenyenzi, ili kuwa nyumba ya kanisa ambapo heshima na upendo na unyenyekevu unatolewa kwa Mwenyenzi. Tujalie, Bwana, kuwa kila mtu anayetembea kupitia hii milango wakati wa hizi siku tano au sita zijazo, atakuwa katika ushawishi kwa namna ambayo hawataweza kuondoka kwenye jengo pasipo kusalimisha moyo wao kwa Kristo. Tunaomba, Baba, kuwa kila mtu mgonjwa anayeingia katika jengo, na hao wanaoingia pamoja na wengine kwenye mioyo yao, wakiomba, kuwa Bwana Yesu mbarikiwa atakuwepo ili kuponya wagonjwa. Jaza kila moyo kwa Roho Mtakatifu.

18 Na, Mungu, wavute hao ndani kutoka kwenye ulimwengu uliolewa, wenye uMendo wa kichaa cha dhambi, wenye kupenda anasa za ulimwengu, kabla ya kuchelewa sana, kabla milima haijasawazishwa, kabla hasira kuu ya Mungu haijamwagwa juu ya kizazi kisichoamini. Mungu, lilete hilo karibu nasi zaidi wiki hii kwamba tuweze kuona hilo, na mioyo yetu itajazwa mno, hadi kila mtu ndani hapa atafanyika kuwa mhudumu barabarani na jirani, ili kuwaleta wengine kwa Kristo.

Sisi hatujui kama tutawahi kumaliza huo uamsho hapa, au hapana, hadi Wewe utakapokuja. Lakini tunajua hili jambo moja, kuwa siku fulani Wewe utakuja, na sisi hatujui hiyo itakuwa saa ipi. Lakini hebu sisi tuishi kila saa kwamba, kama ilikuwa ile saa, sisi tutakuwa tayari kwenda kusimama katika Uwepo Wako, ili kusikia hilo likisemwa, "Hilo umetenda vema, mtumishi wangu mwema na mwaminifu; ingia katika furaha za Bwana, zilizoandaliwa kwa ajili yako tangu msingi wa ulimwengu." Tunajiweka wakfu wenyewe, pamoja na hili jengo, na Neno Lako, kwa heshima na utukufu wa Mungu, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

19 Bwana awabariki. Sasa tunatamani kusoma Andiko fulani hapa, linalopatikana katika Kitabu cha Mtakatifu Yohana, sura ya 12 na aya ya 20.

Na hoja yetu-yetu katika hili, hoja yetu, kuchanachana ... hoja ya kampeni yetu ni kwamba "Yesu Kristo ni yule jana, leo, na hata milele na milele." Sasa, hiyo ni Waebrania 13:8, "Yesu Kristo ni yule jana, leo, na hata milele na milele." Sasa Mtakatifu Yohana 12:20.

...Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda... sikukuu:

Basi hao walimwendea...Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, Bethsaida ya Galilaya, na wakamwomba, wakisema, Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.

20 Sasa, natamani kutoa sasa, kwa dakika chache zijazo, mazungumzo madogo ya kawaida, kuweka msingi na kurejea nyuma. Tunakwenda kuanza, kama ilivyokuwa, juu ya uponyaji wa Kiungu. Na siku zote, Yesu, mimi naamini, katika huduma Yake, kama asilimia themanini ya hiyo, ilikuwa juu ya uponyaji wa Kiungu.

Na kama ambavyo rafiki yangu mwema wa kale, Ndugu Bosworth, ambaye wengi wenu Wakristo mlimfahamu, yeye alizoea kusema, "Siku zote, ili kumkamata samaki, huwaonyeshi ndoana, unawaonyesha chambo. Na samaki ananyakua chambo, na kupata ndoana."

Hivyo ndivyo tunavyojaribu kuwadaka Wakristo kwa ajili ya Kristo, ni kwa njia ya miujiza ya uponyaji wa Kiungu, ili kuonyesha Uwepo Wake. Na ndipo, kwa vile, wao wanajua kuwa mtu hawezi kufanya hayo mambo, hivyo hilo linaidaka nafsi ya mwaminio, na yeye nalikubali hilo juu ya hiyo misingi. Hivyo sasa, kwa kuanzia, mimi nataka kutoa mazungumzo ya kusema kuwa Yeye ni yule jana, leo na hata milele na milele.

Na hawa Wayunani walisema, "Mabwana, tunataka kumwona Yesu."

21 Sasa, hao Wayunani wangelielezea mawazo yetu vizuri haMa jioni hii. Mimi siamini

kwamba kuna mtu hapa isipokuwa ambaye angelitaka kumwona Yesu. Ili kupata tu idadi ndani hapa ambao waliwahi kusikia juu Yake, wangeMenda kumwona Yeye, nataka tu wewe uinue juu mkono wako. Ona tu, ni asilimia mia moja. Hakuna mtu ambaye aliwahi kusikia juu Yake ... Hilo Jina la kupendeza tu hutufanya sisi tutamani kumwona Yeye!

Kuna kitu fulani juu ya Kristo ambacho hakiko kwa mtu mwingine. Yeye alikuwa tofauti. Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Na kuna-kuna kitu fulani tofauti mno juu Yake ambacho mtu mwingine haonekani kuwa nacho kama Yeye alivyokuwa nacho. Nasi tunaye Roho, eleweni, lakini tunaye Huyo kwa kipimo, Yeye anaye Huyo pasipo kipimo, Yeye alikuwa Imanueli, Mungu akiishi katika Mwili wa Kristo Yesu, Mungu alidhihirishwa katika mwili. Kristo alikuwa mfano wa Mungu uliodhihirishwa, akimweka wazi Mungu kwa watu. Kile Mungu alichokuwa, wao walikiona katika Kristo, Mwana Wake. Yeye alikuwa mpakwa Mafuta. Neno Kristo humaanisha "mpakwa Mafuta."

22 Na sasa kama hao Wayunani, wakiwa wanamtafuta Yeye...Sasa, sasa hebu tuweke juu ya kila Neno. Hao Wayunani, wakiwa wanamtafuta Yesu, walikuja kwa mmojawapo wa wanafunzi Wake, ambaye alikuwa FiliMo, wa Bethsaida. Na yeye-yeye alikuwa anamtafuta Yesu, hivyo yeye akaja kwa mwanafunzi, na yule mwanafunzi akampeleka kwa Yesu. Kama hiyo ilikuwa ndiyo njia ya kumwona Yesu, kwa hao Wayunani, na sisi tuna shauku ya kumwona Yesu yule yule, na Biblia inasema, "Yeye ni yule jana, leo, na hata milele na milele," basi kwa nini sisi tusimwone Yeye? Sasa ninyi...

Maandiko hayawezi kusema uongo. Hayo ni ile Kweli. Mimi naamini hilo. Na kama haya Maandiko yalikuwa makosa, basi mimi ningelikuwa ninafanya jambo fulani lingine jioni hii mbali na kusimama hapa nikilileta Hili. Lakini mimi ninaamini kuwa Hayo ni sahihi, sahihi kabisa. Hayahitaji fasiri yoyote. Hayo yako tu jinsi yanavyopasa kuwa, yameandikwa tu kwa usahihi ndani hapa, kwa sababu Mungu ameona kwenye hilo kuwa Hayo yalidumu namna hiyo. Sasa tazama.

23 Ni wangapi wanaoamini kuwa Mungu hana ukomo, mwenye enzi yote, aliyeko kote, anayejua yote? Hakika. Yeye ni Mungu, kwa hiyo uamuzi Wake wa kwanza juu ya chochote inapasa ubakie vile vile, kwa sababu maamuzi Yake yalikuwa makamilifu, kwa sababu Yeye hawezi kufanya kitu chochote isiMokuwa kikamilifu. Hilo ndilo tu lote yeye alilo, ni ukamilifu. Kamwe Yeye hawezi kubadilika. Sasa hapa ndipo matumaini yetu yalikojengwa juu ya Neno. Kama Mungu aliwahi kuita kwenye sehemu ya tukio, ili kufanya uamuzi juu ya kitu fulani, uamuzi Wake wa kwanza inapasa ubakie vile vile milele na milele. Kamwe hauwezi kubadilika. Kabla tu hatujafikia hilo, wazia hili.

24 Wakati Mungu, katika Bustani ya Edeni, Yeye alipoitwa kwa ajili ya ukombozi wa Adamu na Hawa, Yeye alikuwa na tiba moja, hilo lilikuwa damu. Na kamwe Yeye hajabadilisha hilo. Milele na milele, hiyo-hiyo ni damu! Kamwe Yeye hawezi kubadilisha hilo.

Mungu alipoitwa pale, ili kuponya mtu aliye mgonjwa, Yeye alimponya kwa imani yake. Na kamwe Yeye hawezi kulibadilisha hilo. Unaona? Na kama yeye alimponya mtu mmoja, kwa sababu ya imani yake katika Mungu ili kufanya hilo, basi Yeye itampasa aponye anayefuata, au Yeye alitenda kwa makosa Yeye alipomponya wa kwanza, na Yeye alitenda kwa makosa Yeye alipomwokoa wa kwanza. Unaona? Hivyo wewe huwezi...

Sisi tunabadilika. Sisi ni-sisi ni kile mnachokiita "chenye ukomo." Na Yeye hana ukomo. Hivyo Yeye hawezi kubadilika, kwa sababu Yeye ni mkamilifu. Sisi tunatoa uamuzi, halafu tunatazama, "Vema, hilo lilikuwa makosa. Nitalifanya hilo namna hii, liwe bora zaidi." Lakini siyo Yeye. Lile la Kwake la kwanza lilikuwa kamilifu. Hivyo ndivyo hilo linapasa libakie daima. Hivyo Yeye hawezi kujifunza zaidi au awe mwerevu zaidi, kama ambavyo sisi huwa tunawaza, lakini Yeye ni mkamilifu tangu mwanzo.

25 Sasa tunasikia mno juu ya Yesu katika hizi siku, na kokote unakokwenda. Sasa, mimi ni mmishenari, mnaelewa; huu ni mzunguko wangu wa saba. Sasa, hili katika viwanja vya misheni, tunakuta watu wakiabudu sanamu na kadhalika, na mamilioni yao. Lakini hapa katika Amerika tunakuta makanisa kwenye kila kona, kila moja linamzungumzia Mungu kwa njia fulani, na wanakuta maoni mengi mno mbalimbali ya Hilo. Baadhi hujaribu kumMata Mungu kupitia njia moja, na lingine nyingine. Kwa kweli kuna njia iliyo sahihi mahali fulani. Ni lazima Mawe na njia iliyo sahihi mahali fulani.

Kwa sababu, kama Daudi alivyosema, "Wakati kilindi kinaMoita Kilindi, ni lazima kwanza pawepo na kitu fulani kinachoitia huo wito, au huo wito kusingekuwepo pale."

Katika maneno mengine, inaMasa pawepo na Muumbaji kabla ya kuweza kuwepo maumbile. Unaona? Inapasa pawepo Kitu Fulani kilichoweka uumbaji ndani yako, kabla; Muumbaji kuweka uumbaji, na ndipo inapasa pawepo na kitu fulani cha kuitikia hilo. Kabla hapajakuweko pezi juu ya mgongo wa samaki, inapasa pawepo na maji kwanza kwa ajili yeye kuogelea ndani, la sivyo yeye asingelikuwa na pezi. Kabla hapajakuweko na mti kukua katika dunia, inapasa pawepo na ardhi, kwanza. Na maadam kuna njaa katika moyo wa mwanadamu, kwa ajili ya Mungu, inapasa pawepo Mungu mahali fulani ili kuitikia huo mwito.

Na wengi wako hapa jioni hii wakitafuta uponyaji wa Kiungu. Kwa nini mnautafuta huo? Kwa sababu kitu fulani ndani yako kinakuambia wewe, "Kuna Chemchemi mahali fulani." Unaona? Na maadam kuna kitu fulani ndani yako, kinachokuambia, "Kuna Chemchemi mahali fulani," inapasa hiyo Chemchemi iwepo, la sivyo kamwe hapatakuweMo na shauku ndani yako. Unaona, Muumbaji, ili kuumba maumbile.

26 Sasa tunakuta watu katika siku hii, wakitamani, wakivuta, wakitembea hapa na pale, wakitafuta, wakinyakua, wakibadili makanisa, wakibadilisha makaratasi na madhehebu mbalimbali, na kadhalika. Tatizo ni nini? Kuna njaa kwa ajili ya Kitu Fulani, lakini wao hawaonekani kama kwamba wanaweza kupata kile wanachoonea njaa. Inapasa kiwepo hicho Kitu mahali fulani.

Sasa, baadhi leo hii humtafuta Mungu kupitia kanuni zao za imani. Baadi ya watu wanafikiri, kwa kupitia kanuni zao za imani, wao "Watapitia tu kwenye kanuni fulani ya imani, wanayompata Mungu." Baadhi hufikiri, "Kujiunga na madhehebu fulani, humpata Mungu."

27 Vema, Yesu alikuta kitu kile kile Yeye alipokuja duniani. Aliwakuta Mafarisayo, Masadukayo, na wengine, mipangilio mbalimbali, au mashirika ya dini na kanuni za imani za siku ile. Yeye aliwaambia nini wao? "Kwa mapokeo yenu mmezifanya Amri za Mungu zisiwe na nguvu." Unaona?

Mimi nafikiri huko kumtafuta Mungu kupitia kanuni ya imani au kwa kujiweka kimafumbo, kitu Mekee hilo linachofanya, hilo linarejesha hilo moja kwa moja nyuma, na hulikana Neno, linarejea moja kwa moja nyuma na kufanya Amri za Mungu zisiwe na nguvu. Kwa mfano, unajaribu kumtafuta Mungu katika kutamka Imani ya Mitume. Na ndipo unarejea nyuma kuMata Marko 16 ifanyike halisi kwako, "ishara hizi zitawafuata hao waaminio"; mbona, wao watakuambia wewe kwa haraka, "Vema, hizo siku za miujiza zimekwishakupita!" Ndipo hilo linafanya nini? Hilo linahitaji Amri za Mungu na kuzifanya zisiwe na nguvu; unaona, hazina nguvu, Amri za Mungu.

Amri Yake ilikuwa "Enendeni ulimwenguni na kuhubiri Injili kwa kila kiumbe." Sasa, Injili ilikuja siyo kwa Neno pekee, bali kupitia udhihirisho wa Neno, madhihirisho ya Roho Mtakatifu yakifanya Neno kuwa hai. Unaona, ni Roho akilipeleka Neno.

28 Neno lilikuwa wazo. Na wazo ni...Neno ni wazo lililodhihirishwa, unaona. Sasa, Hilo lilikuwa mawazo ya Mungu, kile Yeye alichokuwa anakwenda kukifanya, basi Yeye alikidhihirisha hicho kwenye Neno.

Na sasa wakati Roho Mtakatifu anaMolishikilia Neno, Yeye hulifanya hilo litukie na hulidhihirisha Hilo, hulifanya Hilo kuwa halisi, kila Neno la Mungu. Hakuna Andiko isipokuwa kile ambacho kimetolewa kwa uvuvio! Na kila Neno la Mungu ni kamilifu na sahihi, na Hilo litatimia. Kila Neno lazima litimie. "Mbingu na nchi zitapita," Yesu alisema, "lakini Maneno Yangu hayatashindwa." Kila Neno la Hilo lazima litimie.

Sasa, basi Mungu anapofanya hilo, na tunapata kanuni zetu za imani basi, kama sisi tukisema kanuni fulani za imani au mambo fulani ambayo sisi ni wa hayo...Na mimi sina chochote kinyume na hilo. Hilo ni sahihi.

Ni kama tu kula tikiti maji, kama yule mtu mweusi alivyosema yeye alipokula kipande chake. Yeye alisema, "Wewe utawaza nini juu ya hilo, Mose?"

Yeye akasema, "Hilo lilikuwa zuri, lakini kwa kweli kuna ya zaidi ya hilo." Hivyo, hilo halikutosha kutosheleza.

29 Kanuni ya imani ni sawa, lakini hiyo haitoshelezi tu hadi ufikie chini kwenye Neno. "Na mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kile Neno litoalo kinywani mwa Mungu." Hilo ndilo mtu ataishi kwalo. Neno la Mungu ni mkate wa kiro wa mwanadamu, ni neno la Mungu lililodhihirishwa.

Na wakati Mungu alipowapa Israeli nchi ya ahadi, wao hali walipokuwa wangali bado katika Misri, iliwapasa wao wapiganie kila inchi ya hiyo nchi. Mungu alimwambia Yoshua, katika Yoshua 1, "Kila mahali zitakapokanyaga nyayo za miguu yenu, nimewapa ninyi kumiliki." Hivyo nyayo za miguu humaanisha "kumiliki." Baadhi ya watu wanaweza tu kufika kwa shida pembezoni mwa hiyo nchi. Baadhi wanaweza kuchukua upanga wenye mikono miwili na kukatisha njia yao kupitia Wafilisti na Waamori hadi wawe wamechukua hicho kitu chote. Hilo ndilo tungepaswa kufanya. Kila ahadi ni kwa ajili yetu. Tuna ... Nyayo za miguu ni umiliki. Unakwenda moja kwa moja na kuichukua hiyo! Mungu alitupa sisi hiyo. Hiyo ni ahadi na ni Kweli, na ni kwa ajili yetu.

Sasa, basi katika hizi kanuni za imani, wao wanakuja pale tena, kama ninavyosema, na kufanya, kwa mapokeo yao, Amri za Mungu zisiwe na nguvu. Huondoa hilo, huelezea hilo kote.

30 Lakini kwa kweli kuna njia fulani ya kujua kiMi ni cha kweli, kwa sababu Andiko hapa linasema, "Yeye ni yule jana, leo na hata milele na milele." Sasa, wewe huwezi kuchukua hilo Andiko na kuliondoa kwenye Biblia. Inakupasa kuliacha hilo katika Biblia, kwa sababu hilo ni la ndani mle. Na kama Hilo linasema, "Yeye ni yule yule," hilo halimaanishi Yeye ni yule yule kwa sehemu, hilo linamaanisha kuwa "Yeye ni yule jana, leo, na hata milele na milele."

Sasa, basi, sisi tunataka kuona. Ningependa kumwona Yeye akiingia ndani ya jengo jioni hii. Ningependa kumwona Yeye. Sivyo wewe? Tulisema kitambo kidogo kilichopita, tungependa. Tungependa kumwona Yeye. Vema, basi, kama Yeye alituahidi hilo, kwa nini sisi tusipende? Hilo ni ninii...Sasa, kama tutafungua tu macho yetu na akili zetu kwa kitambo kidogo tu, mimi naamini kuwa tutaelewa, na Yeye ataingia ndani na kujionyesha Mwenyewe kwetu. Sasa, na ndipo tutaondoka jioni hii, tukisema, "Tutamwona Yesu."

31 Ni wapi wao walikompata Yesu katika Agano la Kale; pale pale katika Agano Jipya, mimi namaanisha? Pale pale kwenye Neno, kwa sababu Yeye alikuwa Neno. Sasa, Yeye hakuwa Neno katika njia ambayo wao wameiweka pamoja, bali Yeye alikuwa katika Neno katika njia ambayo Mungu aliiweka pamoja, kwa sababu Yeye alikuwa Neno lililo hai.

Sasa, Yeye aliMokutana na Shetani, Yeye alikutana na yeye kwenye Neno. Yeye-Yeye-Yeye alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili; lakini Yeye alipokutana na Shetani kamwe Yeye hakutumia nguvu Zake za Uungu Wake, kile Yeye alichokuwa. Yeye alisema, "Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu.' Imeandikwa, 'Wewe utamwabudu Bwana Mungu wako, na utamtumikia Yeye Meke Yake.'" Yeye alipokutana na Shetani, Yeye alikutana na Yeye kwa Neno, kwa sababu Yeye alikuwa Neno. Sasa, Neno lilifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu. Sasa, Musa alinena juu Yake Yeye katika Neno, sasa, katika Kumbukumbu la Torati, ile sura ya 18, aya ya 15.

32 Musa aliandika vile Vitabu vitano vya Agano la Kale. Kutoka na Mwanzo; Mwanzo, Kutoka, Walawi, Kumbukumbu la Torati, Hesabu. Yeye aliandika hivyo Vitabu Vitano vya-vya Agano la Kale. Ndani mle, kwa uvuvio kutoka kwa Mungu, yeye aliandika na kusema kilichokuweko, ndipo yeye akaandika na kutuambia kitakachokuweko. Na kile yeye alichosema kingekuweko, kilitukia; hivyo sisi tunajua kuwa kile Yeye alichosema kilikuweko, ni kweli. Kwani mtu anaweza kutazama njia hii na aone kile kinachokuja kutukia, na kinakuja kutukia, basi kile yeye alichosema nyuma kule kilikuwa hakika cha uvuvio Mia.

33 Sasa, Wayahudi wote walifundishwa kuamini manabii wao. Bado wanafanya hivyo. Kama Paulo alivyosema, "Wayahudi wanatafuta ishara, na Wayunani hekima, na kadhalika. Sisi tunamhubiri Kristo aliyesulubishwa."

Sasa, Biblia ilikuwa imewafundisha hao Wayahudi, "Kama kuna mmoja miongoni mwenu aliye wa kiroho, au nabii, Mimi Bwana nitajijulisha Mwenyewe kwake, katika unabii na maono, ndoto, na kadhalika, na kile yeye anachosema kikitukia, basi msikieni yeye." Sasa, hiyo ni akili tu. "Lakini kama hicho hakitatukia kama yeye alivyosema, basi msimsikie yeye." Kwa sababu, Mungu hawezi kusema uongo. Yeye ni Mungu. Lakini kama mtu atasema kitu, na kikatukia, na ndipo mnakiona hicho kikitukia, basi ninyi mnajua kuwa hawezi kuwa huyo mtu. Huyo anapasa awe ni Mungu. Hivyo Mungu aliwaambia manabii...au, aliwaambia Wayahudi kumsikiliza huyo mtu kwa sababu yeye alikuwa nabii kutoka kwa Mungu.

34 Sasa, Musa alikuwa yule nabii mkuu. Hatuna wakati wa kuingia katika maisha yake, ili kuonyesha jinsi yeye alivyofanana na Kristo. Lakini yeye alikuwa nabii mkuu. Na yeye alisema kwamba, Bwana Mungu wako atakuinulia nabii kama Yeye. Itakuja kutukia kuwa yeyote ambaye hatamsikiliza huyu atakatiliwa mbali na watu wake." Sasa, sasa kama Musa alinena, na manabii wengine ... Na Musa, kumbuka, aliandika Mwanzo, Mia. Kutoka Bustani ya Edeni, "Uzao wa mwanamke utakiMonda kichwa cha nyoka," na ahadi zote nyuma kule za kuja kwa Masihi, Musa aliandika hizo. Na ndipo hao manabii wengine, wakuu, kama Isaya, Yeremia, na kadhalika, wote walinena juu ya kuja kwa Masihi. Manabii, ambao, maneno yao yalikuja kutukia. Sasa, wao walinena na kusema Yeye angelikuwa nabii Yeye atakapokuja. "Yeye atakuwa nabii kama mimi," Musa alisema. Hicho ndicho Yeye angekuwa.

Sasa, kama tungelitaka kumwona Yesu leo hii, na Biblia ilisema, "Yeye ni yule jana, leo na hata milele na milele," basi kuna njia moja Mekee ya kufanya hilo. Siyo…

35 Tuweke tu kando kanuni zetu za imani kwa chache, kwa saa moja sasa, au nusu saa. Tuweke kando kanuni zetu za imani, tuweke kando mitazamo yetu ya kidhehebu, na kadhalika, na hebu turejee nyuma na tuone kile Yeye alichokuwa. Sasa hilo lingekuwa…Hilo lingekuwa na mantiki, sivyo? Hilo lingekuwa zuri. Tuende tukaone kile Yeye alichokuwa, na ndiMo tutajua kile Yeye alicho kama tunaweza kuona kile Yeye alichokuwa. Lakini njia Mekee uta…Kama Yeye alikuwa kanuni ya imani nyuma kule, basi kanuni ya imani ni sahihi. Kama Yeye alikuwa dhehebu nyuma kule, basi hilo ni sahihi. Tuone kile dhehebu lilichokuwa au kanuni ya imani ilikuwa nini.

Lakini tunaona, nyuma kule Yeye alikuwa Neno, hivyo Yeye bado ni Neno. Sasa nilisoma kutoka Mtakatifu Yohana. Sasa kama tukifungua nyuma hapa kwenye sura ya 1 ya Mtakatifu Yohana, na sisi tutachukua tu baadhi ya Nani, kile Yeye alichokuwa, kutoka sura ya 1 ya Mtakatifu Yohana. Sasa tunaona kuwa, "HaMo mwanzo kulikuwako Neno," kama ambavyo nimekwishakunukuu, "na Neno alikuwa ndiye Mungu; na Neno alikuwa pamoja na Mungu, na huyo Neno alikuwa Mungu. Na huyo Neno alifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu." Sasa tunaona kile Yeye alichokuwa. Sasa tunalo "Neno likiwa Mungu," Na "Mungu akifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu," katika siku zile. Sasa Biblia ilisema, "Yeye ni yule jana…" Hilo lilikuwa Agano JiMya.

36 Katika Agano La Kale, Kristo, yule yule. Kristo, yule yule katika Agano Jipya. Na Kristo, yule yule, milele na milele. Basi kama sisi tuynaweza kuona "kile Yeye alichokuwa," halafu "kile Yeye amekuwa," na "kile Yeye atakachokuwa," basi tumelipata hilo. Je, hilo ni sahihi?

Musa alisema, sasa, "Yeye atafanana na mimi, Nabii kama mimi." Basi Yeye alipokuja, kile Kristo alichokuwa, iliMasa Yeye awe kile Yeye…Basi ilimpasa Yeye kuwa kile Yeye alichokuwa hapo kabla basi. Hivyo sasa hebu tuanzie pale pale, na ndipo tutaona Yeye atakuwa nini milele na milele. Hiyo ndiyo njia Mekee ya kufanya hilo.

37 Yule yule jana, sasa yupo hapa, tunaona mwandishi wa Waebrania, ni Paulo, akisema, "Yesu Kristo yule jana," akinena na Waebrania. Na sisi sote tunajua kuwa Yehova wa Agano la Kale alikuwa Yesu wa lile Jipya, na ni Roho Mtakatifu wa leo hii. Ni Mungu yule yule tu aliyedhihirishwa tu katika ofisi tatu mbalimbali. Na, hivyo, Mungu yule yule! Na yote yale Mungu aliyokuwa, Yeye aliyamwaga ndani ya Kristo, yote Kristo aliyokuwa Yeye aliyamwaga ndani ya Kanisa. Hivyo, unaona, unaweza kuona kwa haraka kile Yeye alicho, "Yule jana, leo, na hata milele na milele."

38 Sasa, lakini inatupasa tupate asili Yake, kile Yeye alichokuwa. Sasa sote tunajua, na wasomaji wote wa Biblia watakubali, kuwa ile Nguzo ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli jangwani, au wao waliifuata Nguzo ya Moto, ndiyo namaanisha, kwamba huyo alikuwa Malaika wa Agano aliyezungumza na Musa katika kichaka kinachoungua, Nguzo ya Moto ile ile. Wewe, wewe unakubaliana na hilo? Sote tunakubaliana. [Kusanyiko linasema, "Amina."Mh.] Vema, Ni Nani Malaika wa Agano? Kristo. "Musa aliondoka Misri, akihesabu kuwa kushutumiwa kwake Kristo kuwa hazina kuu zaidi kuliko ile ya Misri." Unaona?

Na sasa Yeye alipokuwa haMa duniani, ile Nguzo ya Moto ilifanyika mwili, ikakaa mingoni mwetu. Yeye aliMokuwa hapa duniani, Yeye alisema, "Mimi natoka kwa Mungu, na Mimi nakwenda kwa Mungu." Sasa kumbuka, "jana, leo," unaona. Yeye alitoka kwa Mungu, kutoka kwa Nguzo ya Moto, Yeye anarejea kwa Mungu.

39 Sasa, baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka. Sauli wa Tarso, akiwa njiani

kwenda Dameski, ili kuwakamata watu wa kiMentekoste, akiwa njiani chini kule, kulitukia nini? Nguzo ya Moto, Nuru ilimwangusha yeye. Hakuna mtu mwingine aliyeiona Hiyo. Yeye aliiona Hiyo. Ilimpiga upofu macho yake kwa majira fulani. Hiyo ilikuwa halsi mno kwake; wakati hao wengine wakiwa wamesimama pale, wao hawakuweza kuona chochote; lakini Hiyo ilikuwa inag'aa mno kwake yeye. Ikapofusha macho yake. Na Yeye akasema, "Sauli, Sauli, kwa nini unanitesa Mimi?"

Yeye akasema, "Wewe ni Nani, Bwana?" Sasa sikiliza!

"Mimi ni Yesu. Na ni vigumu kwako kuupiga teke mchokoo." Mnakumbuka hilo. Vema, Yeye huyu haMa, ile ile Nguzo ya Moto iliyokuweko.

Basi kama Yeye ni yule "jana"; basi katika siku ya Paulo, "leo hii"; Yeye atakuwa yule yule "milele na milele"! Hivyo ile nguzo Kuu ya Moto, Mungu, Malaika wa agano, ni yule yule leo hii kama Hiyo ilivyokuwa iliMowaongoza Israeli. Angalia!

Sasa tunakwenda kuanza huduma Yake, katika Mtakatifu Yohana 1. Sisi tunajua…Tutaacha wito na kuzaliwa Kwake, na Yohana Mbatizaji, na tuchukue hadi ubatizo Wake, halafu tuingie jangwani, alipojaribiwa na yule Mwovu, akatoka baada ya siku arobaini mchana na usiku akifunga jangwani. Yeye akarejea na kuanza huduma Yake. Sasa hebu-hebu tuifuate huduma Yake hapa. Kwa haraka, watu walianza kuponywa kutokana na kuombewa, na Yeye.

40 Na tuliona kuwa kulikuweko na mtu kwa jina la Simoni, na yeye alikuja kwa Yesu kwa mwaliko wa ndugu yake, Andrea. Na yeye aliMotembea katika UweMo wa Yesu…Sasa kumbuka, hapa anakuja mtu muhimu. Sasa tunafahamu, kulingana na Matendo sura ya 4, kuwa yeye alikuwa mjinga na mtu asiye na elimu. Tunafundishwa kuwa yeye hakuweza hata kuandika jina lake. Sasa, yeye hakuwa msomi. Yeye hakuwa askofu. Yeye hakuwa-kuhani. Yeye alikuwa mvuvi.

Mungu siku zote huchukua kitu fulani ambacho si chochote, na kufanya kitu fulani kuitokana na hicho. Yeye hujidhihirisha Mwenyewe kupitia kitu ambacho si chochote, ili kwamba mtu yeyote aweze kuona ni Mungu. Unaona, Yeye huchukua kitu fulani ambacho si chochote.

Na yeye alimchukua huyu mtu mjinga. Sasa Yeye anakwendaje kumfanya huyu mtu ajue kuwa Yeye ndiye? Bila shaka, kulikuweko wengi wa kuigiza waliokuwa wameMita. Na tulikuwa nao kuMitia vile vipindi.

41 Na unapochukua dola ya bandia, na kuitazama hiyo dola ya bandia, wewe unakumbuka tu kuwa hiyo dola ya bandia imetenegezwa kutokana na dola halisi. Kwani kama hapakuweko na dola halisi, basi hiyo ya bandia ingelikuwa nakala halisi. Unaona? Hivyo maadam unamwona mtu fulani akiigiza au akitimiza wajibu wa mnafiki, kumbuka tu kuna Mkristo halisi mahali fulani. Unaona? Unamwona mtu fulani akitambulisha aina fulani ya mfumo wa kidini wa mungu wa uongo, au aina fulani ya nguvu ya kimiujiza, dini, kazi ya kiakili, kumbuka tu, nyuma Male, mahali fulani, kuna Mungu wa kweli aliye halisi. Tazama. Ee, mimi nalipenda tu hilo! Angalia.

42 Sasa mara tu, mara tu Simoni … Hebu tuchukue igizo dogo la Simoni huko nyuma, kwa dakika moja, akiwa mzee. Baba yake alikuwa mtu mzee, pia. Na labda huenda siku moja, kama ninavyosoma habari ndogo ya kwake; baba yake alikuwa mvuvi, na yeye alikuwa anavuta ndani. Wao walikuwa wanahitaji samaki, mno. Hivyo wao, siku ile walipata samaki wengi. Siku zote wao waliomba kabla ya kwenda kuvua samaki. Na hivyo yeye alikuwa na madeni ya kulipa, na yeye alivua kundi kubwa la samaki. Na yeye akaketi chini kando ya mtumbwi na kuweka mkono wake kumkumbatia Simoni, na kusema, "Simoni!"

Jina lake lilikuwa Yona, unajua. Na yeye akasema, "Simoni, mvulana wangu, nimewaza kuwa siku fulani nitamwona Masihi. Hilo limekuwa tumaini la watu wetu tangu tutoke Misri, au tangu tujue kulikuweko na Masihi aliyeahidiwa. Miaka elfu nne imekwishakupita, mwanangu. Watu wengi wakuu, manabii, wamekufa, wakimtazamia Yeye. Mimi niliwaza Yeye angelikuja katika kizazi changu. Lakini mimi ninazeeka sasa, labda mimi sitamwona Yeye. Lakini, Simoni, nataka wewe ukumbuke, wewe na Andrea, kuwa huenda Yeye akaja katika kizazi chenu, kwani mimi ni mzee sasa na niko tayari kwenda kuwa na watu wangu. Na mimi nimejaribu kuwalea ninyi wavulana katika usahihi, nimejaribu kuwalea kwenye Neno.

"Sasa sikiliza. Sasa, Simoni na Andrea, kabla huyo Masihi kwa kweli hajainuka,

kutakuweko na mambo mengi yatakayoendela chini ya jina la 'Masihi,' kwa sababu hao watakuwa adui. Lakini usisahahu, Simoni, wewe na Andrea siku zote dumuni na Neno. Msiliache Neno. Kumbuka, Masihi atakuwa nabii kama Musa, kwani hiyo ni kamili. Haidhuru, huenda yeye ni mtu mkuu wa kidini, na yeye huenda akaweza kueleza maneno, yeye huenda akaweza kufanya chochote kama hicho; lakini Biblia ilisema, 'Yeye atakuwa Nabii kama Musa.' Amina. Sasa hivyo ndivyo mtakavyomjua Yeye."

43 Na siku ile Simoni alipokuwa akitembea, na Andrea, katika Uwepo Wake, na Yesu akiwa amesimama pale, Ambaye Andrea alikuwa amemwambia Simoni, "Tumemwona Masihi."

Na ningeliwazia Petro aliwaza namna hii, au Simoni, kama yeye alivyokuwa wakati ule, "Sasa labda umezama hadi mwisho wa kilindi, Andrea. Mimi nitakwenda kule pamoja na wewe, nami nitajua."

Hivyo yeye alipofika mbele ya Yesu, Yesu alisema, "Jina lako ni Simoni, na wewe ni mwana wa Yona."

Hilo lilitosha. Lilikuwa ndilo hilo. Yeye alimwamini Yesu na kumkubali Yeye, kwa namna ambayo yeye alikuwa na funguo za huo Ufalme baadaye. Yeye hakwenda shule yoyote au chochote, yeye alikuwa na funguo za huo Ufalme. Kwa sababu, kwa ufunuo wa Mungu yeye alijua kuwa yule alikuwa Masihi, kwa sababu ilikuwa ni Masihi wa Kimaandiko. Yeye alikuwa nabii, na wao hawakuwa na nabii kwa miaka mia nne, tangu Malaki. Wao walikuwa wamekuwa na manabii wa uongo. Lakini, nabii halisi aliyesema ile Kweli! Na hapa alikuweko Mtu akiwa amesimama hapa Ambaye, mara tu Yeye lipomwena yeye, siyo tu alimjua yeye alikuwa nani, bali alijua baba yake mzee mtauwa alikuwa ndiye aliyemfundisha yeye. Hilo lilimaliza hilo! "Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu." Unaona?

"Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona." Hilo lilitosha kumwonyesha yeye. Sasa hilo ndilo Yesu alilofanya jana, ili kujithibitisha Mwenyewe, kuwa Yeye alikuwa Masihi.

44 Kulikuweko na mmoja aliyekuwa amesimama pale. Tutaharakisha. Kulikuweko na mmoja aliyekuwa amesimama Male, kwa jina la Filipo. Mbona, hilo lilimsisimua yeye! Huyo ndiye ambaye tunamsoma hapa. Hilo lilimsisimua yeye mno! Sasa, Filipo huenda alisema, "Sema, hilo, hilo linatosha! Sasa nina hakika!"

Yeye akaenda pale kilimani, maili kumi na tano. Yeye alikuwa na rafiki ambaye alikwenda naye shuleni, mtu mwema, mtu wa Maandiko, mtu mwadilifu, mtu aliyejua Andiko, na kumpenda Mungu. Na mimi naweza kumwona yeye akibisha hodi mlangoni [Ndugu Branham anagonga juu ya mimbara-Mh.] na-na kusema, "Nathanaeli yuko wapi?"

Mke wake akasema, "Yeye yuko nje katika-uani pale. Yeye anaomba.

Yeye akaenda kumtafuta, na Nathanaeli alikuwa chini ya mti. Naye alipompata, alisema, "Njoo, umwone tuliyempata; Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu."

45 Na sasa naweza kumuwazia Filipo au… Nathanaeli akisema, "Sasa, Filipo, panaweza kuwepo kitu chochote kizuri kutoka Nazarethi?"

Yeye akasema, "Njoo uone."

Sasa, hilo ni tamko zuri kwa mtu yeyote. Usikae nyumbani na kukosoa. Usisimame na kutoka nje. Ukae na usubiri, na uone kama hiyo ni ile Kweli au hapana. Unaona? "Njoo, ujionee mwenyewe."

Vema, wakazunguka kwenye kona Male; hebu tuwazie juu ya mazungumzo yao. Naweza kumsikia Filipo akimwambia Nathanaeli, "Nathanaeli, Andiko linasema Masihi atakuwaje?"

"Ee, Yeye atakuwa-Yeye atakuwa Nabii kama Musa."

"Hakika. Hilo ni sahihi. Vema, huyu Yesu wa Nazarethi ninayekuambia juu Yake, je, unakumbuka yule mvuvi mzee uliyenunua samaki kutoka kwake, na yeye hakuweza kuandika jina lake?"

"Ndiyo. Ee, hakika, mwana wa Yona. Namfahamu yeye vizuri. Jina lake ni Simoni."

"Mara tu alipoingia katika Uwepo wa huyu Mtu, Yeye alimwambia yeye alikuwa nani, na juu ya baba yake. Hilo halikunishangaza mimi kuwa Yeye hakukuambia wewe ni

nani," yeye anasema.

"Vema," yeye akasema, "sasa, subiri kwa kitambo kidogo. ItaniMasa nimwone huyo."

46 Vema, hatimaye, wao wakafika kwenye mkutano. Mara yeye alipofika katika Uwepo wa Yesu, Yesu alisema, "Tazama, Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake."

Sasa huenda wewe ukawa umesema, "Vema, hakika, Yeye anajua yeye ni Mwisraeli, kwa jinsi yeye alivyovalia." Watu wote wa Mashariki wanavaa kwa kufanana, wote ni hali ya weusi, na wao wana sharafa, na kilemba, na-na majoho, na kadhalika, sawasawa tu. Na Yeye angelijuaje yeye alikuwa mtu mwaminifu na mtu wa haki, asiye na hila?

Yeye akasema, Yeye akamwambia, "Tazama, Mwisraeli ambaye ndani yake hamna hila."

Na hilo lilimshangaza yule mtu wa Kimaandiko. Yeye akasema, "Rabi," ambalo humaanisha mwalimu, "lini Wewe uliwahi kunifahamu mimi? Hii ni mara yetu ya kwanza kukutana. Lini Wewe uliwahi kunifahamu mimi?"

Yeye akasema, "Kabla Filipo hajakuita wewe, wewe ulipokuwa chini ya mti, Mimi nilikuona." Hilo ndilo lenyewe. Ndilo hilo. "Mimi nilikuona wewe," maili kumi na tano kuzunguka mlima, jana yake. "Mimi nilikuona wewe ulipokuwa chini ya mti." Sasa, unajua yeye alifanya nini? Yeye alimkimbilia Yesu, akasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu! Wewe ni Mfalme wa Israeli!" Hiyo ndiyo ile saa! Kwa nini? Yeye ni wa Kimaandiko, Yule ambaye nabii alisema kuwa angekuja. "Wewe ni Mwana wa Mungu! Wewe ni Mfalme wa Israeli!" Kile hao wengine walichosema hakikuleta tofauti yoyote.

47 Sasa, kulikuweko na hao waliokuwa wamesimama pale, ee, Mafarisayo na Masadukayo, na maaskofu, na chochote kingine zaidi, kiongozi, viongozi wakuu wa kidini, makuhani wakuu, na makuhani, na wengine zaidi, wakiwa wamesimama pale, nao wakamtazama Huyo. Wao walijua iliwapasa wao wawajibike kwa kusanyiko lao. Iliwapasa wao kuwapa wao swa-…walikuwa na jibu kwa kusanyiko lao. Hivyo, unajua kile wao walichosema? Wao walisema, "Huyu Mtu ni Beelzebuli." Unaona? Katika maneno mengine, "Yeye ni mpiga ramli, pepo." 119

Na Yesu akawageukia, na kusema, "Nitawasamehe ninyi." Unaona, wao walimwita Roho wa Mungu, aliyekuwa akifanya hilo, roho mchafu. Akasema, "Mimi nitawasamehe kwa kufanya hilo. Lakini siku fulani Roho Mtakatifu atakuja kufanya kitu kile kile, na neno moja dhidi Yake kamwe halitasamehewa katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao." Neno moja dhidi Yake. Sasa, hilo lilikuwa kwa ajili ya kipindi kingine. Watazame wao.

48 Sasa, Biblia ilisema kuwa, "Neno la Mungu," Waebrania 4, "ni upanga mkali kuliko upanga wenye pande mbili. Neno, ambaye ndiye Kristo, kali zaidi ya upanga ukatao kuwili, ukikata hadi kwenye mafuta ya kwenye mfupa, na Mtambuzi wa mawazo na makusudio ya moyo." Neno! Neno linapokwenda mbele Lenyewe, Hilo ndivyo lilivyo. Hiyo ni taarifa, huo ni udhihirisho wa Neno. Na kulikuweko Neno likiwa limesimama Male, lililofanyika mwili miongoni mwao, likifanya hasa kile Hilo lilisema lingefanya, na wao hawakulitambua Hilo.

49 Sasa, kumbuka, kuna jamii tatu pekee za watu duniani, nao ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafeti. Sisi tunajua hilo, kama tunaamini Biblia. Wote walianzia kutoka kwao watoto watatu, watoto wa Nuhu; Myahudi, Mataifa, na Msamaria.

Je, ulimwona Petro akiwa na funguo za ule Ufalme? Ule wa kwanza yeye alioufungua, ulikuwa Wayahudi, Menye Pentekoste. Je, hilo ni sahihi? Na Filipo alipokwenda chini na kuhubiria Wasamaria, wao walikuwa wamebatizwa katika Jina la Bwana Yesu, lakini hawakuwa wamempokea Roho Mtakatifu bado; nao wakatuma na kumtaka Petro aje chini na kuweka mikono juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Je, hilo ni sahihi? Matendo 10:49, "Petro aliponena haya Maneno, Roho Mtakatifu akashuka juu yao hao waliosikia hilo Neno." Unaona? Sasa watazame hao watu watatu: Wayahudi, Mataifa, na Wasamaria.

50 Sasa hapa Wayahudi na Wasamaria walikuwa wanamtafuta Masihi. Sasa Yesu alikuwa njiani Mwake kwenda Yeriko, kutokea Yerusalemu kwenda Yeriko, lakini Yeye alihitaji kupitia Samaria.

Sasa kumbuka Mtakatifu Yohana 5:19, Yesu alisema, baada ya kupita kisima cha Bethesda, "Amin, amin nawaambia, Mwana hawezi kufanya lolote Mwenyewe, bali kile Yeye aonacho Baba akifanya." Je, mlilipata hilo? Yesu alisema, "Mwana hawezi kufanya chochote Mwenyewe," hiyo ni Yeye, "bali kile Mimi," siyo kumsikia Baba, bali, "aonacho Baba akifanya." Sasa, hilo Andiko liko sahihi, au hayo mengine huenda yakawa makosa. Yeye alisema, "Kabla Mimi sijafanya chochote, Mimi naona kwa ono kile Baba anachonionyesha Mimi nifanye, na ndipo nakwenda kufanya hicho." Unaona? Hilo lilikuwa limemzunguka tu Yeye. "Lakini ninyi, hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba." Hilo ni kweli.

Hivyo Yeye alihitaji kwenda Samaria, na Yeye alikwenda juu kule Samaria. Na ilikuwa ni kama saa sita. Na Yeye alituma wanafunzi Wake ndani, Yeye alipokuja kwenye mji wa Sika, na Yeye akawatuma wanafunzi Wake ndani ili kuchukua akiba ya chakula, chakula. Nao walipokuwa wameondoka, mwanamke wa Sika akatoka.

51 Sasa, yeye alikuwa mwanamke ambaye tungeweza kumwita "mwanamke mwenye sifa mbaya," labda mwenye sura nzuri, mwanamke kijana aliyechukua njia ya makosa, naye alikuwa akiishi kimakosa. Naye akatoka kuja kuteka maji. Bila shaka, yeye hawezi kutoka nje…Mimi nimekuwa katika ile nchi mwenyewe, na desturi zao bado ni zile zile. Mwanamke wa aina ile hashirikiani na wanawake waadilifu; hivyo yeye hawezi, yeye hawezi kuja kisimani wakati huo huo wao wakiwa pale, au chochote. Na hivyo-hivyo yeye akaja kisimani baada ya hao wengine kupata maji yao, yeye akatoka kuja kuteka maji.

Na yeye alipofanya, akasimama, na alikuwa akiteremsha kwa kamba, inapasa ishike kwa ndoana, na kuiweka tu kwenye mshikio wa chungu namna hii. Hiyo siyo ndoo; ni aina ya chungu, kama, kilichotengenezwa kutokana na udongo, nao wanakiteremsha chini kisimani, na kukivuta juu kwa kamba. Na hivyo yeye akaanza kuteremsha ile ndoo chini, na yeye akasikia Mtu Fulani akisema, "Mwanamke, niletee Mimi maji." Na yeye akatazama Male. Ilikuwa ni kama picha ya igizo hii hapa, ambaMo watu wa mji wanakuwa nje Male, kutoka Sika. Na ndipo yeye akatazama pale, na pale akawa ameketi Myahudi wa umri wa makamo. Sasa, kwa kweli Yeye alikuwa na kama umri wa miaka thelathini na mbili tu.

52 Lakini yeye alikuwa amekwishakupita tu, katika Mtakatifu Yohana 6, pale ambapo wao walimwambia Yeye alionekana kama kwamba alikuwa na umri wa miaka hamsini. Lakini, bila shaka, kazi Yake ilikuwa imefanya hilo, labda. Wakasema, "Wewe siyo Mtu wa umri wa zaidi ya miaka hamsini, na unasema Wewe 'ulimwona Abrahamu'? Sisi tunajua wewe ni mwendawazimu sasa."

Yeye akasema, "Kabla Abrahamu hajakuwako, MIMI NIKO." Hilo ni sahihi. Wao hawakulielewa Hilo, na bado wakiwa wa kidini na werevu walivyoweza. Lakini werevu hauwezi kumjua Mungu; inakupasa kusahau yote hayo, ili kumjua Mungu. Hapana.

53 Nao walikuwa pale. Hivyo huyu mwanamke akasema … Sasa, yeye alikuwa wa kile sisi tunachokiita leo hii, "Malaya," na yeye alikuwa pale. Huyo mwanamke akasema, "Bwana, siyo desturi kwa ninyi Wayahudi kuniomba mimi, mwanamke wa Samaria, kitu fulani, kwa sababu hatuna mahusiano." Kwa maneno mengine, "Kuna utenganisho."

Yeye akasema, "Mwanamke, kama ungejua Huyu uliyekuwa unazungumza na Yeye, ungeliniomba Mimi maji. Ningelikupa wewe maji ambayo hutakuja kuchota hapa." Yeye alikuwa anafanya nini? Kuwasiliana na roho yake.

Sasa kumbuka, Yeye alihitaji kwenda Samaria. Baba alikuwa amesema tu, "Nenda Samaria." Yeye hakufanya lolote hadi Baba amwonyeshe Yeye.

54 Sasa hapa Yeye alikuwa Samaria. Sasa Yeye hajui tu hasa ni nini kinachokwenda kutukia, lakini hapa kuna mwanamke, hivyo Yeye alifikiri angeendelea na mazungumzo pamoja na yeye. Hivyo Yeye akasema, akaendelea kuzungumza juu ya maji. Yule mwanamke akaendelea kuzungumza juu ya kuabudu katika mlima huu au mlima ule, au na kadhalika. Moja kwa moja Yeye akadaka lililokuwa tatizo lake. Ni wangapi wanajua lilikuwa nini? Hakika, yeye alikuwa na wanaume watato, sita, kwa kweli. Hivyo yule mwanamke akasema … Yesu akasema, "Nenda, ukamlete mume wako, na mje haMa."

Yule mwanamke akasema, "Sina mume."

Yeye akasema, "Hilo ni sahihi. Umesema vema, kwani umekuwa nao watano, na yule unayeishi naye sasa siyo mume wako. Katika hilo wewe umesema kweli."

55 Angalia! Sasa inanipasa nizamishe hili ndani, kwa sababu inanipasa kuondoka. Tazama tofauti kati ya yule mwanamke, katika hali hiyo ambayo alikuwa ndani yake, kwa hao wahudumu waliopata elimu ya juu. Yule mwanamke akasema, Bwana, naona kuwa Wewe ni Nabii."

Makuhani na wasomi walisema, "Wewe ni Beelzebuli, pepo, mpiga ramli."

Huyu mwanamke akasema, "Bwana, naona kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua wakati Masihi atakapokuja, Yeye atatuambia mambo haya."

Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, na Yeye ni yule jana, leo, na hata milele na milele, inapasa iwe vivyo hivyo!

Huyo mwanamke akasema, "Sisi tunajua Masihi, ambaye anaitwa Kristo, mpakwa Mafuta; Yeye ajapo, Yeye atatuambia sisi haya mambo. Lakini Wewe ni Nani?"

Yeye akasema, "Mimi Ndiye anayenena na wewe." Hilo lilitosha. Yeye aliliona hilo.

56 Tazama tofauti. Tazama hiyo Nuru ilipomulika juu ya mbegu ya kidini na kanuni ya imani, na kidhehebu, hakufaa kitu hata kidogo. Lakini kwa mara ya kwanza hiyo ilipomulika juu ya ile mbegu ndogo iliyochaguliwa tangu asili pale, Hiyo ilimulika haraka, yeye akaitambua Hiyo. Huyo mwanamke akasema "Bwana, ni lazima wewe uwe Nabii! Sisi tunajua Masihi anakuja, na Yeye atafanya haya mambo."

Yesu aksema, "Mimi Ndiye."

Naye akaondoka, akaingia mjini, akasema, "Njooni, mumwone Mtu ambaye aliniambia mimi mambo niliyoyafanya. Je, huyu siye yule yule Masihi?" Amina.

Hilo ndilo lenyewe! Yesu alikuwa nini jana? Yeye ni yule yule leo hii, na takuweko milele na milele. Unaona? Yeye alikuwako.

57 Daudi alitiwa mafuta kwa Roho wa Mungu. Manabii walitiwa mafuta kwa Roho wa Mungu.

Huyo alikuwa Kristo ndani ya Yusufu, alyemfanya yeye afanane na Kristo kabisa. Aliuzwa kwa viMande thelathini vya fedha, alipendwa na baba, alichukiwa na ndugu, katika hii nyumba ya gereza. Kama Kristo alivyokuwa juu msalabani, mmoja aliokolewa; na mchinja nyama na mwandaa meza, na mmoja aliokolewa na yule mwingine alipotea, kitu kile kile. Aliketi mkono wa kuume wa Farao; na kila wakati alipokwenda mbele, baragumu ilipigwa, "Kila mmoja apige magoti, Yusufu anakuja." Hakuna mtu aliyeweza kufika kwa Farao, isipokuwa kupitia kwa Yusufu pekee. Huyo alikuwa Kristo ndani ya Yusufu!

58 Huyo alikuwa Kristo ndani ya Daudi, kama mfalme aliyekataliwa, na kwenda juu ya Mlima wa Mizeituni, yeye alipokuwa ameondolewa kwenye ufalme chini pale na watu wake mwenyewe, na mfalme aliyekataliwa, alikwea kwenye kilele cha kilima na kuililia Yerusalemu, na kulia, kwa sababu yeye alikuwa mfalme aliyekataliwa. Roho yule yule ndani ya Kristo aliililia Yerusalemu, na kusema, "Yerusalemu, Yerusalemu, nitakufunika kwa mbawa mara ngapi kama kuku afanyavyo."

Ilikuwa ni Kristo ndani ya hao watu, wapakwa mafuta, wakija juu hadi huyu Mpakwa mafuta mkamilifu alipokuja. Dhabihu kwa ajili ya dhambi haikufanyika. Yeye hakuweza kuja katika mwili wote namna ile, kwa sababu ilikuwa tu chini ya…Wao walipakwa mafuta. Lakini sasa Roho Mtakatifu amekuja, ambaye ni Kristo katika umbo la Roho. Sasa tazama.

59 Sasa, kwa nini Yeye akufanya hizo ishara kwa ajili ya Mataifa? Hiyo kamwe haikufanywa na Yeye. Kwa nini? Mataifa walikuwa hawamtazamii Masihi. Wao walikuwa makafiri, sisi tulikuwa makafiri, watu wetu, Warumi na kadhalika, nyuma kule tukiwa na rungu mgongoni mwetu, tukiabudu sanamu. Wao walikuwa hawamtazamii Masihi. Na Masihi huja tu kwa hao wanaomtazamia Yeye. Hiyo ndiyo njia pekee. "Kwa hao wanaomtazamia, Yeye atawatokea kwa mara ya pili." Hao tu wanaomtazamia Yeye! Siyo tu hawa ambao wanafungamana; bali hao ambao wanamtazamia Yeye kwa uhalisi. Na tazama, kamwe Yeye hakuja kwa Mataifa. Ule muujiza kamwe haukufanyika mbele ya Mataifa.

Na Mungu asiyebadilika! Sasa tumekuwa na miaka elfu mbili ya elimu na aina zote za vitu, na sasa umekuja wakati wa jioni, na sasa Mataifa wanatazamia Masihi anayekuja. Sasa, kama Yeye ni yule yule! Yeye alitukia hivyo hivyo wakati ule, kwa hayo

makabila mawili. Inampasa Yeye kutokea kwa njia hiyo hiyo Male. Na kuahidi, ijapokuwa! Andiko moja zaidi, na nitafunga.

Siku zote kumbukeni, wekeni madaraja matatu ya watu katika akili zenu. Siku zote wao wako pale, ambao ni: waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini. Wao wako katika kila kundi. Unaona?

60 Na Abrahamu alipewa ahadi, na uzao wa Abrahamu baada ya yeye. Sasa utazame uzao wa Abrahamu, katika mfano wa Lutu, alikwenda chini katika Sodoma, anasa za ulimwengu; hilo ni kanisa la kimwili, dhehebu, shirika la dini. Lakini Kanisa la kiroho, ambalo lilikuwa Abrahamu ambaye Mungu alimtembelea kibinafsi, lililoitwa, kamwe yeye hakwenda katika Sodoma, yeye alikuwa nje ya Sodoma; hilo ni Kanisa, lililoitwa. Sasa, wakati wa mwisho ulikuja, wakati Yeye alikuwa anakwenda kuangamiza nchi kwa moto.

Hilo ndilo Yeye analojiandaa kufanya tena. Je, hilo ni sahihi? Sasa tazama. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa penye kuja kwa Mwana adamu." Kumbukeni, hayo yalikuwa mataifa ya Mataifa. Unaona? Ule mwisho, kama ilivyokuwa katika Sodoma. Sasa hapa kuna Mataifa wakija. Wakati wa Wayahudi uliangamizwa na maji. Wakati huu, Mataifa wanaangamizwa kwa njia ya-kwa njia ya moto. Tazama, "kama ilivyokuwa katika Sodoma," hebu tutazame tu.

61 Pale alikuweko Abrahamu, Kanisa teule, lililoitwa litoke Sodoma; la kiroho, Mungu akiwatokea katika kambi yao wakati wote, ishara na maajabu, pamoja na ahadi. Akiwa ameketi hapa juu ya vilima, ardhi kame, wasio na utajiri na kama hao wengine; lakini masikini, wakiwa wameketi; kundi dogo lililodharauliwa, lilodhihakiwa. Hao wengine walikuwa wametoka na kuwa matajiri, na watawalaji wa mji, kama watoto wa Kaini walivyofanya siku zote, watu wakuu, wanasayansi, madaktari, na kadhalika. Wao walikuwa hapo, kama ambavyo ilikuwa siku zote. Mungu habadiliki. Nao walikuwa wameketi Male.

Sasa, chini katika Sodoma kulikuweko na kanisa vuguvugu, Lutu na kundi lake. Abrahamu na kundi lake walikuwa Kanisa teule. Tazama. Na kisha Wasodoma, wasioamini.

62 Na palikuja Wajumbe watatu kutoka Mbinguni, waliovalia kama wanaume. Na Abrahamu aliketi mlangoni mwa hema lake asubuhi moja, na kutazama, na wakaja Wanaume watatu. Sasa, wao walikuwa na vumbi kwenye nguo zao, kama ambao walikuwa wamesafiri. Na Abrahamu, kulikuweko na Kitu Fulani kidogo chini ndani yake, yeye alijua kuwa hao walikuwa watu wasio wa kawaida. Wao walionekana kama watu fulani ambao yeye alipaswa kuwajua, hivyo yeye akakimbilia nje.

Kuna kitu fulani juu ya Mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili, unapokutana naye! Nilikuwa ninakuja kupitia mgahawa leo hii, mtu fulani akasema, "Mungu akubariki." Nikageuka nyuma. Mimi nikasema, "Loo, kitu Fulani cha makosa." Bibiye mdogo akanishika mkono. Sasa, kitu fulani juu ya Mkristo aliyezaliwa mara ya pili!

Na hawa Malaika wakaenda juu pale na kuanza kuzungumza na Abrahamu. Sasa kumbukeni, wawili wa hao walikwenda chini katika Sodoma, ili kuita, waone kama waliweza kupata watu kumi wenye haki. Je, hilo ni sahihi? Wawili wa hao waliondoka. Mmoja wao alibaki nyuma na kuzungumza na Abrahamu. Je, hilo ni sahihi? Sasa tazama.

63 Chini pale, hapakuwepo na miujiza, ni kuwapiga tu hao upofu wao walipoingia ndani. Na kuhubiri Injili humpiga upofu asiyeamini. Hilo ndilo Biblia inalosema. Na kumbukeni, Billy Grahamu wa kisasa na wasomi chini kule wakiwa wanahubiri. "Tokeni! Tokeni! Tokeni!" Unaona?

Lakini kumbukeni, Yule aliyebaki nyuma na Abrahamu, alifanya kitu kingine na Kanisa teule, Yeye alikuwa ameketi akiwa amegeuzia hema kisogo. Sasa kumbukeni, yeye alikuwa amekuwa "Abram" hadi siku moja au mbili tu kabla ya hilo, na Sara alikuwa "S-a-r-a-i." Lakini sasa yeye ni S-a-r-a, na yeye ni A-b-r-a-h-a-m-u; "baba wa mataifa," na "malkia." Unaona? Sasa huyu Mgeni alijuaje? Na Yeye akasema, "Abrahamu, mke wako yuko wapi?" Yeye alijuaje yeye alikuwa ameoa? Yeye alijuaje jina lake lilikuwa Sara?

Na Abrahamu akasema, "Yeye yuko ndani ya hema nyuma Yako."

Sasa tazama. "Mimi," kiwakilishi binafsi, "Mimi nitakutembelea wewe." Yeye alikuwa amefanya nini? Aliketi pale na kula nyama ya ndama ambayo Abrahamu alimwua, akala

mkate ambao Sara alikuwa ameoka, na kunywa maziwa kutokana na ng'ombe.

64 Mtu Fulani aliniambia siyo muda mrefu uliopita, akasema, "Huyo alikuwa Nani, Ndugu Branaham?"

Mimi nikasema, "Ilikuwa ni Mungu."

Abrahamu alipaswa kujua, yeye alizungumza na Yeye. Muulize mhudumu yeyote. Alimwita Yeye, "Elohimu," aishiye Mwenyewe.

Sasa tazama, usilikose hilo. "Abrahamu, mke wako yuko wapi, Sara?" Akasema, "Yeye yuko ndani ya hema, nyuma Yako."

Akasema, "Mimi nitakutembelea wewe kulingana na wakati wa maisha." Kile Yeye alichomwahidi yeye miaka ishirini na tano kabla ya hilo! Abrahamu alikuwa na umri wa miaka mia, na Sara alikuwa na umri wa miaka tisini. "Mimi nitakutembelea kulingana na maisha."

65 Sasa kumbukeni, Sara, mwanamke mzee, ilikuwa imekoma kuwa na yeye kama mke. Hakuna mwanamke wa umri wa miaka tisini…Huenda miaka ishirini au ishirini na tano, labda, tangu yeye awe mke kwa Abrahamu. Wao walikuwa wazee. Naye akacheka moyoni mwake; unajua, kile tunachoita, kucheka kwa siri." Akasema, "Mimi, mwanamke mzee kama mimi nilivyo; na bwana wangu, Abrahamu, nje pale, mzee, pia; na mimi niwe na furaha kama bibiarusi tena, pamoja na Abrahamu?" Na yeye akacheka kuhusu hilo.

Na yule Malaika, akiwa amepiga hema kisogo, akasema, "Kwa nini Sara amecheka, akisema hilo, "Haya mambo hayawezekani'?" Huo ulikuwa ni aina gani ya uwezo wa kusoma mawazo?

66 Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa penye kuja kwa Mwana adamu." Pale, kanisa lisilo halisi lilikuwa na wajumbe. Na Mjumbe wa Roho Mtakatifu yupo pamoja na Kanisa teule, akifanya kitu kile kile, ambacho humfanya Yeye, Kristo yule jana, leo, na hata milele na milele. Ni nani Mjumbe wa saa hii? Hakuna mwanadamu! Roho Mtakatifu ndiye Mjumbe wa saa hii. Hicho ni kitu gani? Mungu, akikaa ndani ya mwili wa mwanadamu. Utukufu! Najisikia wa kidini. Amina. Mungu, katika mwili wa mwanadamu, akikaa miongoni mwenu!

Yesu alisema, "Tazama, bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena (huyo ni asiyeamini); bado ninyi mtaniona Mimi (Kanisa), kwani Mimi," kiwakilishi binafsi tena, "Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa kipindi, mwisho wa ulimwengu." Yesu Kristo ni yule jana, leo, na hata milele na milele! Mungu wetu hajafa! Yeye anaishi milele na milele! Yeye anaishi mwishoni mwa wakati, wakati jua linazama.

67 Jua siku zote huchwa katika Mashariki na hutua katika Magharibi. Ustaarabu umesafiri pamoja na jua. Sisi tunajua hilo. Ustaarabu wa zamani zaidi tulio nao ni China. Na Mwana (M-w-a-n-a) alipotoa mwanga kwa mara Yake ya kwanza, ilikuwa juu ya watu wa Mashariki. Sasa ustaarabu umesafiri hadi sisi tuna…Moja kwa moja kule ni Pwani ya Magharibi! Kama tukienda mbali zaidi, tutakuwa Mashariki tena, kama tukiendelea mbele zaidi. Ustaarabu umesafiri pamoja na-pamoja na jua.

Sasa nabii alisema, "Kutakuweko siku ambayo haiwezi kuitwa mchana wala usiku, yenye majonzi, siku yenye ukungu." Watu wamejua vya kutosha juu ya Mungu kujiunga na kanisa, kuweka jina lao kwenye kitabu, wanatembea katika ile Nuru waliyokuwa nayo. Katika siku yenye ukungu, kuna nuru mno ya jua, la sivyo hungeliweza kutembea popote hata kidogo. Lakini yeye alisema, "Katika wakati wa jioni, kutakuwako Nuru." Hicho ni kitu gani? Jua lile lile linalokuchwa Mashariki, linatua Magharibi. Na yule yule Mwana wa Mungu aliyedhihirishwa na kutokea Mashariki, anatokea Magharibi sasa kwenye wakati wa jioni, Nuru ya jioni kwa Kanisa lililoitwa na kujazwa kwa Roho Mtakatifu.

68 Kristo, kwa njia ya Damu na Nguvu za mishipa Yake Mwenyewe, alitakasa watu walio wachafu, na kukaa miongoni mwao katika umbo la Roho Mtakatifu. Amina. Ile picha Ya Huyo, ni wangapi waliowahi kuiona hiyo picha? Iko pale pale nyuma sasa. Unaweza kwenda na kuitazama hiyo. George J. Lacy, mkuu wa Shirika la Upelelezi katika alama za vidole na mengine, zimechukuliwa. Na huyo huyo Malaika aliyewaongoza Israeli, yupo hapa sasa akitenda na kufanya kitu kile kile Yeye

alichotenda wakati Yeye alipokuwa katika Utu wa Yesu Kristo. Kristo, ule mwili, umepaa juu kwenye mkono wa kuume wa Baba; lakini Roho Mtakatifu akarudi, ule Uzima uliokuwa ndani ya Kristo, uko ndani ya Kanisa. Sasa Kristo haku- …Vema, kama…

69 Yesu aliposema, katika Yohana 15, "Mimi ni Mzabibu, nanyi ni matawi." Sasa, Mzabibu hauzai matunda; ni tawi. Mnajua hilo, ninyi watu hapa, ninyi wakulima wa zabibu, na kadhalika. Sasa, kama hilo tawi la kwanza lililotoka kwenye Mzabibu, lilizaa Kitabu cha Matendo nyuma yake, hilo Kanisa la kwanza; kama huo Mzabibu uliwahi kuchipua lingine, tawi lingine, hilo litaandika Kitabu cha Matendo kingine nyuma yake. Kwani, Uzima ule ule ulio ndani ya Mzabibu huleta ndani ya tawi. Hakika. Tunayo matawi mengi yaliyopandikizwa ndani hapa.

70 Niliona mti siku ile nyingine katika Phoenix, Arizona, ulikuwa na matunda tisa mbalimbali juu yake. Matunda. Na mimi nikamwambia mtu fulani, nikasema, "Ndugu Sharrit." Mimi nikasema, "Ndugu Sharrit, hiyo ni, ni nini hicho? Limao, chenza, balungi, na-na tunda la zabibu, na kila kitu." Nikasema, "Sasa wakati hilo, yote hayo yanachumwa," nikasema, "mwaka ujao ndiMo utazaa, utazaa machungwa, kwa sababu huo ni mti wa mchungwa."

Akasema, "Loo, haMana. Huo utazaa tunda la zabibu, limao, na chochote kile hilo tawi lilicho."

"Mbona," mimi nikasema, "hicho ni kitu cha ajabu. Wewe unamaanisha ulipotosha huo mti wa mchungwa kuwa aina hizo za miti?"

Yeye akasema, "Hapana. Mchungwa bado ni ule ule. Kama huo utawahi kuchiMua tawi jingine, hilo litazaa chungwa. Lakini kile kilichopandikizwa ndani yake namna hiyo, hicho kinazaa cha aina yake, kwa sababu hilo ni tunda la jamii ya machungwa."

Mimi nikasema, "Hilo ndilo lenyewe."

Dhehebu linaweza tu kuzaa tunda la dhehebu. Lakini kama huo Mzabibu wa asili utawahi kuchipua lingine, hilo litakuwa Yesu Kristo yule jana, leo, na hata milele na milele! "Mimi nitarejesha," asema Bwana. Amina. (Ni wakati wa kwenda nyumbani.)

71 Nini? "Mabwana, tutamwona Yesu." Ni Mtu wa aina gani unayemtafuta. Mtu wa aina ile ile aliyekuwa. Sasa, huendi chini barabarani hapa na kumtafuta mtu aliyevaa aina fulani ya joho, na makovu ya msumari kukatisha kichwa chake, au chochote kile. Mnafiki yeyote anaweza kufanya hilo. Na hilo ni sahihi. Mtu yeyote anaweza kuigiza hilo. Lakini itakuwa ni ule Uzima uliokuwa ndani ya Kristo, utakuwa ndani ya Kanisa Lake. Ndio huo, ule Uzima!

Kama ukichukua uzima kutoka kwenye boga, na kuuweka huo ndani ya zabibu, huo utazaa maboga, kama ungeishi namna hiyo. Hakika, ule uzima ndani yake.

Na hapo ndipo Uzima ulipo sasa. Uzima wa Kristo ndani ya Kanisa, huzaa Kristo tena. Hivyo ndivyo wao wanavyomwona Kristo. Ile … Katika Yohana 14:12, yeye alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, siye anayejifanya kuamini; bali yeye aniaminiye Mimi, matendo niyatendayo yeye atayatenda pia. Zaidi ya haya yeye atayatenda, kwani Mimi nakwenda kwa Baba Yangu." Yesu Kristo yule jana, leo, na hata milele na milele.

72 Wakristo, Nikiwa mmishenari, nimewaona mamia ya miungu mbalimbali, ndiyo, maelfu ya hao, aina zote, Shiite, Jains, Buddha, aina zote hizo nyingine zikiwekwa pamoja, unaona. Mimi niliburudishwa hapa siyo muda mrefu uliopita, katika India pale nilipokuwa na umati wangu mkuu zaidi, elfu mia tano katika kusanyiko moja, na pale niliburudishwa katika hekalu la Jains. Na ndani mle kulikuweko na dini kumi na saba mbalimbali, miungu kumi na saba mbalimbali, na kila mmoja wa hao ni kinyume na Ukristo. Lakini, ee, jamani, unapaswa uwe umemwona Yeye akija kwenye sehemu ya tukio. Kila mmoja wa waanzilishi wao amekufa na kuondoka. Wa kwetu alifufuka tena na Yeye yuko hai milele na milele, akiwa anaishi katika Kanisa Lake, yule jana, leo, na hata milele na mielle.

73 Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

Bwana Yesu, tuna furaha mno kuzungumza juu Yako. Wewe ni wa kupendeza mno na wa kustahili heshima mno kwa yote tuwezayo kusema. Lakini, Baba, Neno moja tu kutoka Kwako lingefanya zaidi ya yote mimi niliyowahi kusema, au mhudumu mwingine yeyote. Neno moja tu kutoka Kwako litamaliza hilo. Je, Wewe hutafanya hilo jioni hii, Baba, tunaMosubiri sasa, kwa kitambo kidogo tu, kwa yenu, mimi ninaomba. Sisi tuta,

sisi tutasubiri siyo kwa kitambo kidogo kwa ajili Yako, Bwana, tutasubiri hadi Wewe uwe tayari. Sisi tunataka kusikia kutoka Kwako. Naomba, Baba wa Mbinguni, jioni hii, kama ambavyo nimelishikilia kusanyiko tena, kwa muda mrefu. Lakini wao ni wapendwa mno, Bwana. Nami najua jua la jioni limeondoka. Sisi tunaishi tu katika vivuli sasa. Na, Mungu, huenda pakawepo mtu fulani ambaye hakujui Wewe. Naomba kwamba Wewe utakuja kwetu jioni hii, Bwana, katika umbo la Roho Mtakatifu, na uruhusu watu wakuone Wewe, waone Yesu yule yule ambaye walimwona katika siku zilizokwishakupita.

74 Haikuwa mwanadamu, mwili (wao walisulubisha huo, bali Mungu aliufufua huo), lakini huo ulikuwa Uzima uliokuwa ndani Yake. Yeye hakusema, "Njoo, muone jinsi Mimi nilivyovaa nguo Zangu, hiyo ni ishara kuwa Mimi ni masihi. Njooni, muone zile shule ninakotokea, kanuni ya imani ninayofundisha." Hapana, hilo halikuwa lenyewe, jinsi Yeye alivyojitambulisha Mwenyewe. Lakini Yeye alisema, "Kama sifanyi matendo ya Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini kama ninafanya matendo ya Baba Yangu, na ninyi hamniamini Mimi, aminini matendo hayo, hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Hayo ndiyo yanayonifanya Mimi nijulikane." Nao waliona kuwa Wewe ulikuwa Masihi, kwa sababu Wewe ulikuwa Nabii, Mungu-Nabii.

Na sasa jioni hii, tunaomba kuwa Wewe utatubariki jioni hii kama Wewe ulivyowafanya KleoMa na rafiki yake. Baada ya wao kutembea Mamoja na Wewe kwa miaka mitatu na nusu, na kuwa wameona hayo mambo ambayo Wewe ulitenda; ndiMo Wewe ukasulubishwa, chini ya Pontio Pilato-Pilato, Wewe uliteseka, ukasulubishwa, ukafa. Na kwenye siku ya tatu, wao walikuwa njiani mwao kuelekea Emau. Wao walikuwa wamesikia tetesi kwa wanawake na baadhi ya wanafunzi, kuwa "Yeye alikuwa amefufuka." Lakini siku ile Wewe ulitembea Mamoja nao na kuzungumza nao kwa matendo siku nzima. Wao hawakukujua Wewe.

Huenda wengi hapa wamefanya. Wewe umetembea na wao na kuzungumza na wao, nao hawakulitambua Hilo.

75 Lakini jioni ilipokuja, wao walikukaribisha Wewe ndani, na Wewe ukafunga milango na kuketi chini. Ndipo Wewe ukafanya kitu Fulani jinsi tu Wewe ulivyofanya hilo kabla ya kusulubishwa Kwako. Wao walijua wakati huo ilikuwa ni Wewe. Kitambo kidogo, Wewe ukatoweka kutoka mbele yao, ukatoka na kuingia gizani. Wao wakaondoka na kwenda kwa watu wao, wakisema, "Bwana amefufuka!"

Mungu, je, Wewe utafanya hilo jioni hii tena? Fanya jambo fulani miongoni mwetu jioni hii, kama tu Wewe ulivyofanya hilo kabla ya kusulubishwa Kwako. Ndipo sisi tutakuwa na ujasiri na kujua kuwa Kristo wetu hajafa, bali Yeye amefufuka kutoka kwa wafu, na yuko hai miongoni mwetu, milele na milele. Tunajisalimisha wenyewe Kwako, Baba. Nalisalimisha hili kanisa Kwako, na kila roho ndani hapa, Kwako, kuwa Wewe uweze kututumia sisi ili kumheshimu Kristo. Katika Jina la Yesu naomba hilo. Amina.

76 Sasa kabla hatujaomba au kuita mstari wa maombi, ninakwenda kuwahitaji ninyi jambo moja. Nataka kila mtu, tafadhali, kushikilia kiti chako kwa dakika chache tu. Sasa ni lazima uwe mnyenyekevu wakati huu. Sasa, kama wewe huamini, basi toka nje kwa urahisi hasa. Lakini sasa, kama unakwenda kuamini, keti kwa utulivu, kumi na ta-…kama dakika kumi na tano, unaona. Hebu tuone kama Yeye atanena nasi. Sasa sisi, hatuko katika…Tuko katika eneo, lakini hili ni kanisa. Umewekwa wakfu kwa ajili ya kusudi hilo, hivyo hebu tuketi kwa utulivu hasa. Kila mmoja wenu ni roho. Kama wewe siyo roho, umekufa. Uanona? Hivyo basi wewe ni roho, na basi Roho Mtakatifu anaposhuka chini ili kuMaka mafuta miongoni mwa watu, Yeye huwasiliana, anachukua hizo roho, unaona. Na wewe ukitembea, kuna kuhama.

Wewe unasema, "Ee, Ndugu Branham!" Vema, kwa nini Yeye aliwaongoza vipofu nje ya mji? Na, hivyo, unaona? Unaona?

Sasa ni wangaMi wanaomwamini Yeye? "Mabwana tutamwona Yeye."

77 Sasa tunao mstari mdogo wa maombi tunaokwenda kuita. Naamini wao wanaita … Wapi uli … Au yeye alitoa, naam, kadi za maombi moja hadi mia? Moja hadi mia, nini? C, C. Vema, hebu tuite baadhi, kadi za maombi. C, namba moja, ni nani aliye na hiyo kadi? C, namba moja. Tazama kadi yako ya maombi, wewe uliye na kadi yako ya maombi. Namba moja. Vema.

Unakwenda kuwaleta hao kwa njia ipi, njia hii, nyuma njia hii? Vema.

C, namba moja. Namba mbili. Vema, bibiye. Namba tatu. Namba tatu. Kama unaweza kusimama, au uinue mkono wako au kitu fulani kingine, hivyo niweze…Namba tatu, nani aliye na kadi ya maombi? Bwana, vema. Namba nne, kadi ya maombi namba nne. Vema. Vema, namba nne. Ni nani alye na namba nne, uinue mkono wako, tafadhali? Vema,bibiye, njoo hapa. Unaona, wao tu…

78 Wao wanakuja chini, yule mvulana anafanya, na kuchukua hizi kadi za maombi na kusimama mbele yako. Yeye anazichanganya pamoja, ndipo yeye anaanza kukupa wewe kadi ya maombi. Unaweza kupata sita, na yule mwingine anapata kumi na nne.

Njoo haMa, bibiye. Nne, tano. Na basi ni nani aliye na tano, inua mkono wako. Kadi ya maombi namba tano. Na ndipo kitu kingine wakati yeye…Moja kwa moja chini hapa, bibiye, hii. Na ndipo kitu kingine wao wanachofanya katika hilo, ndipo wakati mwingine naita kutokea sehemu moja…Ni wangapi waliowahi kuwa katika mkutano hapo kabla, mojawapo ya mikutano yetu? Ee, vema, mimi nilifikiri nilikuwa miongoni mwa wageni. Hakika siyo. Vema. Tano, sita. Nani aliye na sita? Vema. Saba, nane, nane, tisa. Napata hili, kwa sababu viziwi, na watu wako katika viti vya magurudumu na hawawezi kutembea. Tisa, kumi, namba kumi. Kumi, tunatamkaje hilo katika Kihispania? Kumi. Vema, kumi na moja, kadi ya maombi kumi na moja. Nilifikiri mtu fulani katika roshani…Hapa. Vema, kumi na mbili. Vema, kumi na mbili. Kumi na tatu. Kadi ya maombi kumi na tatu, je, unayo hiyo, bibiye? Kumi na nne, kumi na nne, kumi na tano. Hebu, vema, hebu tuanze namna hiyo sasa. Vema.

79 Sasa, tafadhali, sasa uwe tu mnyenyekevu . Sasa ni wangapi ndani hapa ambao hawana kadi ya maombi, na bado unaamini kuwa Yesu Kristo atakuponya? Inua mkono wako. Mimi sijali pale ulipo. Ni wangapi wamekuwa katika mikutano hapo kabla, na wanajua kuwa kuna wengi walioponywa nje kule kuliko walivyo juu hapa, kwa kuwaita tu hao? Hakika, pasipo kadi za maombi? Uwe tu na imani sasa, usitie shaka, amini kwa moyo wako wote.

Kadi ya maombi namba tano inakosekana. Bawabu anaita kadi ya maombi namba tano. Unaona, kama utasimama na…Usichukue kadi ya maombi isipokuwa unakwenda kuitumia hiyo; unaona, usichukue. Uchukue namba yako sasa, kwa sababu tunakwenda kuomba kwa ajili ya kila mmoja aliye na hizo kadi, unaona, na hatu-hatutaki ninyi mkose wakati wenu. Kwa sababu, sasa, tunapoita tena sasa, tuliachia kwenye kumi na tano, hapo ndipo tutaanzia labda kesho jioni, mahali pale pale, unaona. Tutakuwa nazo, kila mmoja, hivyo basi uta-utakosa muda wako. Unaona? Naam. Kadi ya maombi namba tano. Vema.

80 Na uwe tu na imani. Usitie shaka. Na amini kwa moyo wako wote. Sasa, sasa kila mmoja wenu sasa mlio na kadi ya maombi, au usiye na kadi ya maombi, na unaamini, sasa wanaoandaa mstari, tazama upande huu sasa.

Wakati mmoja kulikuweko na mwanamke, na huenda yeye hakuwa na kadi ya maombi, lakini yeye alikuwa kile kilichohitajika, imani. Na yeye alipita kukatisha kusanyiko, na yeye akasema, "Kama naweza tu kugusa vazi Lake, nitakuwa mzima." Ni wangapi waliowahi kusikia habari hiyo? Yule mwanamke aliyekuwa na kutokwa damu. Sasa yule mwanamke masikini alidhamiria kuwa yeye alikuwa anakwenda kumgusa Yesu. Yeye akasema, "Mimi namwamini Yeye. Mimi sijali ni makuhani wangapi na hao wengine hawamwamini Yeye, mimi namwamini Yeye. Na naamini kama nitaweza kugusa vazi Lake, nitakuwa mzima. Mimi naamini Yeye ni masihi." Je, wewe unaamini Yeye ni Masihi?

81 [Kusanyiko linajibu, "Amina! Amina!"-Mh.] Hakika. Sasa unaweza kumgusa Yeye? Sasa, kwa wahudumu, ndugu wahudumu wako wapi? Vema, mhudumu, sasa…Je, Biblia inasema, ndugu mhudumu, au ninyi nyote wasomaji wa Biblia, kuwa, "Yeye sasa hivi," Kitabu cha Waebrania, sura ya 3, "ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na hisia za madhaifu yetu"? Ni wangapi wanajua Biblia inasema hilo? Hakika. Vema, basi, kama Yeye ni Kuhani Mkuu, na Kuhani Mkuu yule yule, je, Yeye hatatenda hivyo hivyo? Unaona? Kama Yeye ni yule jana, leo, na hata milele na mielle, (hilo ndilo somo letu), Yeye angetenda hivyo hivyo. Sasa unasema…

82 Sasa kama utakuja juu hapa na uniguse mimi, halingeleta tofauti yoyote. Ukigusa wachungaji, halingeleta tofauti hata kidogo. Umguse mchungaji wako hapa, yeyote yule, halingeleta tofauti hata kidogo. Lakini, mguse Yeye!

Basi wewe utajuaje ulimgusa Yeye? Yeye angelifanya kazi pale pale na kufanya kitu

kile kile. Unaona? Mguse Yeye na uone kama Yeye hatanena moja kwa moja kupitia hapa, na aseme, "Imani yako; ulikuwa na kitu zulani," na chochote kile, na kukuambia kilikuwa kitu gani, na nini kilitukia, na yote kuhusu hilo. Sasa, ni wangapi waliona hilo likifanyika mara mia, inua tu mkono wako. Unaona? Hakika, halikushindwa kamwe, halikushindwa kamwe. Kwa nini? Yeye hawezi kushindwa; Yeye ni Mungu. Unaona? Je, huna furaha kuwa Mkristo, Mkristo halisi, aliyezaliwa mara ya pili, kwa kweli mwenye ushindi wa Kristo?

83 Sasa, wewe tu ulioko nje pale katika kusanyiko sasa, uwe tu wanyenyekevu hasa, na useme, "Mimi nitaliamini hilo, haidhuru mtu mwingine yeyote anafanya nini, mtu mwingine yeyote anasema nini, mimi nitaliamini hilo kwa moyo wangu wote." Na uwe tu mwaminifu na uamini sasa. Vema. Vema.

Pale, hao ndugu nyuma kule, na wahudumu na hao, wanawaleta nje wagonjwa.

Sasa mimi nafikiri, ndiyo, hii inatangazwa moja kwa moja. Sasa kama yule kwenye…yule mhandisi kwenye hiyo ataongeza sauti iwe juu kidogo.

Kwa kuwa, wakati mwingine wakati upako unapogonga, basi mimi-mimi huwa sijui kile ninachosema. Unaona, itanipasa ku-…Hilo liko mahali Fulani Mengine nyuma katika maisha, unaona. Na ndiMo mimi ninaMo-…Kama tu wewe ulipoota ndoto hilo, unaona. Na wewe unaota ndoto kama ndoto, kama mimi nikilifanya hilo namna hiyo kwenu, bado ninyi mmesimama papa hapa; na kurejea nyuma kwa miaka kadha, katika maisha ya watu, na kuona kile wao walichofanya, tatizo ni nini, na mengine zaidi, na kulileta hilo namna hiyo, unaona. Na huyo ni Roho Mtakatifu. Basi Yeye anasema kile kilichokuweko, kile kilichoko, na kile kitakachokuweko, na kadhalika. Utazame tu hilo na usikilize kwa makini, na mpate kanda zenu, na Yeye atakuambia.

84 Sasa hapa kuna mtu ambaye labda ni mzee tu kidogo kuliko mimi. Na mimi naamini sisi ni wageni, sisi kwa sisi. Hii ni mara yetu ya kwanza kukutana, kadiri nijuavyo, wewe na mimi, sisi ni wageni sisi kwa sisi. [Yule mtu anasema, "Mimi nimekuwa katika mikutano yako."-Mh.] Wewe umekuwa katika mikutano. Naam. ["Lakini kamwe sijawahi kukutana na wewe."] Yeye amekuwa katika mikutano yangu, yeye alisema, lakini kamwe hajawahi kukutana na mimi. Bila shaka, kuna mamilioni ambao wamekuwa katika mikutano ambao kamwe sikuwajua. Lakini sisi, sasa hapa kuna wanaume wawili wanaokutana kwa mara yetu ya kwanza katika maisha. Yeye ni mwanamume tu akiwa amesimama pale, mimi simjui yeye. Biblia hii hapa; mimi-mimi simfahamu yeye, kamwe sijawahi kumwona yeye katika maisha yangu. Yeye ameniona mimi, kutokea mahali fulani katika kusanyiko, katika mkutano mahali fulani. Lakini yeye amesimama pale.

85 Labda huyu mtu ni mwaminio wa kujifanya. Huenda yeye ni mwaminio. Labda yeye siyo mwaminio hata kidogo, hakuna njia. Huenda yeye ni mwanamume tu. Labda yeye ni mgonjwa, landa yeye siyo mgonjwa. Huenda ni tatizo la nyumbani, tatizo la kifedha. Labda yeye amesimama hapa kwa ajili ya mtu fulani mwingine. Mimi sijui. Lakini yeye amesimama pale, na mimi niko hapa.

"Sasa, mabwana, tutamwona Yesu."

Sasa, mimi ningemfanyia nini mtu huyo? Sasa, naweza kumwendea, niweke mikono yangu juu yake, niseme, "Je, wewe ni mgonjwa, bwana?" Yeye angelisema, "Ndiyo, bwana." Mimi naweka mikono yangu juu yake, niseme, "Utukufu kwa Mungu, haleluya! Nenda, unakwenda kuwa mzima. Haleluya!" Vema, sasa, hilo lingeweza kuwa yeye angekuwa mzima; inategemea kile yeye alichowaza kuhusu hilo. Haidhuru, huenda … Mimi kumtikisa na kuweka mikono yangu ju yake, lisigefanya chochote. Ni imani yake katika Mungu ambayo ingefanya hilo. Lakini, sasa, yeye angeweza kuwa na haki ya kutia shaka hilo.

Lakini kama Roho Mtakatifu anaweza kusiamama hapa na kumwambia yeye jambo fulani ambalo yeye amekuwa, kama Musa alivyoandika katika Mwanzo, basi kwa hakika Yeye angeweza kumwambia kile kitakachokuweko. Yeye angeweza kuamini hilo, sivyo? Sasa, kama Yeye angefanya hilo, kama Kristo angefanya hilo, ni wangaMi wenu mngeamini kwa moyo wenu wote?

86 Unaona, sasa ona, tatizo moja pekee ninaloliona katika Amerika, wao wameona mno hadi wao wanakuwa tu watazamaji, unaona. Usifanye hilo. Mheshimu Kristo, unaona. Usiniangalie mimi. Mimi ni mwenye dhambi niliyeokolewa kwa neema. Lakini

sasa haidhuru Mungu atanipaka mafuta kiasi gani, inamMasa Yeye ampake yeye mafuta, pia. Hilo ni sahihi, hilo lisingefaa kitu chochote. Inampasa Yeye ampake mafuta yeye, Mia. Inampasa Yeye akupake mafuta wewe, unaona, akupake mafuta nje kule, Roho Mtakatifu ashuke juu yenu. 210

Basi, huu ni mkondo tu. Huneni hilo wewe mwenyewe. Yeye hunena kupitia wewe. Ni chombo ambacho Mungu anakitumia ili kunena kupitia hicho, unaona. Ni kama hiki kipaza sauti, kwamba kipaza sauti ni bubu isipokuwa kitu fulani nyuma hapa kinanena kupitia hicho. Na, hicho ni mimi, mimi ninamfahamuje huyo mtu? Kamwe sikuwahi kumwona yeye, lakini mimi ni bubu kwake. Unaona?

87 Hivyo, "Bwana, tutamwona Yesu." Sasa Yeye angefanya nini? Vipi kama huyo mtu ni mgonjwa, Yeye angelisema, "Mimi nitakuponya"? Yeye angeweza kufanya hilo; tayari Yeye amekwishakufanya hilo. Unaona? "Kwa kupigwa Kwake sisi tulipona." Yeye alifanya hilo pale Kalvari. Lakini Yeye angelifanya jambo fulani ili kuonyesha kuwa Yeye bado alikuwa Masihi. Je, hilo lilikuwa sahihi? Vema, basi, Yeye angelifanya nini, Yeye angelisema, "Tazama makovu yangu ya misumari"? Siyo hicho Yeye alichosema hapo mwanzo. Kamwe Yeye…Yeye aliwaambia tu wao kile kilichokuwa ndani ya moyo wao, na kadhalika, nao walijua yule alikuwa Masihi. Sasa huyo ndiye Yeye, yule jana, leo, na hata milele na milele. Je, unaamini hilo? Sema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." -Mh.]

88 Wewe unasema, "Ndugu Branham, wewe unasubiri nini?" Malaika wa Bwana. Hakika. Mimi siwezi kufanya chochote. Namsubiri Yeye. Kama yeye hajanipaka mafuta mimi, mimi siwezi-mimi siwezi kusema chochote. Hilo linategemea tu kile…

Sasa Yeye yuko hapa. Yeye yuko hapa sasa. Na katika Jina la Yesu Kristo nachukua kila roho ndani hapa chini ya udhibiti wangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Mimi sikuji wewe, bwana. Sisi ni wageni. Lakini wewe unaleta jambo fulani…au unatambua kuwa jambo fulani linaendelea. Sasa huyo mtu hawezi kuficha maisha yake. Yeye ni mgonjwa. Mimi siwezi kumponya yeye. Hakuna njia ya mimi kumponya yeye. Huyo mtu amekuwa akienda kwa daktari. Yeye amefanyiwa uchunguzi. Hakika, yeye anatarajia kufanyiwa upasuaji. Hilo ni sahihi. Kama hilo ni sahihi, bwana, inua mkono wako.

Je, unaamini? [Baadhi katika kusanyiko wanasema, "Amina."-Mh.]

89 Unasema, "Ulibuni hilo, Ndugu Branham." Sikubuni. Tazama tena. Tazama upande huu, bwana. Kama tu Bwana wetu akinena na yule mwanamke. Ni Roho Wake. Mimi siyo Yeye. Mimi ni mwanadamu kama wewe, lakini Huyo ni Roho Wake. Chochote kile Yeye alichokuambia, hicho kilikuwa sahihi, chochote. Naam, hili hapa tena. Ndiyo, ndiyo, yeye yuko tayari kwa ajili ya upasuaji sasa hivi, sasa hilo ni tatizo la kibofu na hali ya kuzidiwa. Hiyo ni HIVI ASEMA ROHO MATAKTIFU. Hilo ni sahihi. Inua mkono wako juu kama ni hivyo. Je, wewe unaamini sasa kuwa wewe uko katika Uwepo Wake? Vema. Nenda, ukiamini, na wewe utakuwa mzima.

Amina.

Je, wewe unaamini? Sasa ni jinsi ilivyo tu rahisi kumwona Kristo akitembea.

90 Sasa, bibiye, sisi ni wageni mmoja kwa mwingine. Hapa kuna…Wewe umekuwa katika mkutano. Mimi ninaposema "mgeni," hilo linamaanisha sikufahamu wewe, wewe hunijui mimi. Na mimi…Wewe umeniona katika mikutano, na vitu kama hivyo. Lakini kunifahamu, sema, "Ndiyo, Ndugu Branham, wewe huja nyumbani kwangu, mimi nakufahamu wewe, sisi ni marafiki binafsi," mimi sikufahamu kwa njia hiyo. Na wewe umekuwa tu katika mikutano mahali fulani. Mimi singekuwa na wazo, hakuna chochote juu yako, wewe ni mwanamke tu ambaye amekuwa katika mmoja, aliyehudhuria mkutano fulani mahali fulani. Sasa, kulikuweko na mwanamume. Hapa kuna mwanamke.

91 Hapa kuna picha ya Mtakatifu Yohana 4, mwanamume na mwanamke wanakutana kwa mara ya kwanza katika maisha, kukutana uso kwa uso, kama mwanamke… yule mwanamke wa Samaria na Bwana wetu Yesu. Sasa hapa kuna mwanamke, mimi simfahamu yeye. Kamwe sikuwahi kumwona yeye. Yeye ni mgeni kabisa. Mungu wa Mbinguni anajua hilo. Kamwe sikuwa kumwona yeye. Lakini kama Roho wa Mungu atamwambia yeye yeye yuko hapa kwa ajili ya nini, mtu fulani mwingine au chochote kile, cha nyumbani, kifedha, kile…au ugonjwa au chocote kile, basi itampasa yeye akiri

kuwa kuna Nguvu fulani ya Kiungu haMa ya kufanya hilo. Je, hilo ni sahihi?

Unaona, sasa hilo linategemea kile wewe unachofikiri Hicho ni nini. Unaweza kusema "Beelzebuli" au unaweza kusema "Kristo." Wewe, kama ukisema "Beelzebuli," unaMata thawabu yake. Unaona? Ukisema "Kristo," hiyo ni thawabu Yake. Ni lazima uamini.

Sasa hilo linakuweka mahali gani? Je, mtu fulani anataka kuchukua mahali hapa? Kama wewe huamini hilo, njoo hapa na uchukue mahali Mangu mara moja. [Ndugu Branha anatulia-Mh.] Siku zote kusanyiko linakuwa kimya hilo linapoulizwa.

92 Sasa, dada, tazama upande huu. Kwa nini nilikuita wewe "dada" nilipotazama huku na huku? Nilikuwa nimekugeuzia kisogo. Lakini nilimhisi Roho juu yako, kuwa wewe ni Mkristo. Wewe ni mwaminio. Mimi sikujui wewe, lakini najua wewe ni Mkristo. Kwa sababu, huyo Roho aliye juu yako, na yule Roho aliye juu Yangu, yu jamaa, unaona. Wewe, unajisikia tu kama kwamba umekaribishwa, unajua, kumfanya tu Huyo ajisikie vizuri, umekaribishwa.

Sasa, kama Roho Mtakatifu, kama Yesu alivyokuwa akinena na yule mwanamke pale kisimani, sisi tuko hapa, igizo tu dogo kama kile kisima cha Sikari, nilichokuwa nikizungumza juu yake. Sasa, kwa kuwa sisi wawili ni waaminio, na tumesimama hapa, Roho Mtakatifu akiwa juu yetu wawili. Sasa Yeye alitoa…Mimi siyo mhubiri. Lakini Yeye ananipa mimi karama; hiyo ni kuhubiri kwangu. Hiyo ni karama ya kinabii. Na hizi ni za muda tu; itahitaji imani yako kufanya hilo; kama yule mwanamke aliyegusa vazi Lake, akasema, "Imani yako imekuokoa wewe," unaona. Sasa, hicho ni kitu kile kile kinachohitajika sasa, unaona, inahitaji imani yako. Ndipo Yeye ananiambia mimi jambo fulani, wapi pa kwenda na sehemu fulani.

93 Sasa, hapa, Yeye alihitaji kupitia Samaria. Sasa mimi niko njiani kwenda Alaska, lakini nilihitajika kuja huku. Kwa nini? Nilijisikia kuongozwa kuja hapa. Na mimi niko haMa; wewe umekuja juu hapa jukwaani. Ndilo hilo tu nilijualo. Na wewe umesimama hapa. Wewe ni Mkristo na mimi ni Mkristo, sote wawili tukiwa na Roho Mtakatifu. Na hapa kuna Neno Lake, kuwa Yeye ni yuile jana, leo, na hata milele na milele.

Sasa, kama Yeye atakufunulia kitu fulani kilicho katika maisha yako, wewe utajua kama hicho ni kweli ama hapana. Na Yeye atakufanya wewe uamini basi kwa chochote unachoomba; kwa sababu Mkristo hawezi kusimama Male namna hiyo, wewe una-wewe unahitaji kitu fulani au usingesimama Male.

Je mtu mwingine yeyote ataamini? Je, kuna mtu yeyote anayemhamu yule mtu? Naam, watu wengi wanamfahamu huyo mtu.

94 Vema, kulingana na madaktari, ungepaswa kufanyiwa upasuaji, pia. Ni vivimbe. Hilo ni sahihi. Je, wewe unaamini kuwa Roho Mtakatifu anaweza kunifunulia hivyo vivimbe viko wapi? Ni figo. Hilo ni sahihi. Je, sasa unaamini? Wewe hutokei hapa. Unakuja hapa kutokea kama maili mia mbili au mia tatu. Ulisafiri umbali mrefu kufika hapa. Hilo ni sahihi. Hilo ni sahihi. Na, hata hivyo, wewe ni mke wa mhudumu. Je, unaamini Mungu anaweza kuniambia mimi wewe ni nani? Je, hilo lingekusaidia? Bibi Johnson. Nenda, ukiamini, na uwe mzima; na kwa moyo wako wote.

Je, unaamini kwa moyo wako wote? Unaona? Yesu Kristo! Mabwana, tutamwona…Unasema, "Inakuwaje hilo?" Vema, hilo siyo zaidi ya lile Yeye alilowaambia hao wengine. Je, unaamini? "Mabwana, tutamwona Yesu." Huyo ni Yeye. Sasa nenda uzungumze na huyo mwanamke, umwulize yeye.

95 Sasa hapa kuna mwanamume, mgeni kabisa, mimi simfahamu yeye, kamwe sikuwa kumwona katika maisha yangu. Huenda yeye ameliwa na saratani, yeye anaweza kuwa na matatizo ya nyumbani, ya kifedha. Mimi sijui yeye ana shida gani. Yeye amesimama hapa, mwanamume tu. Sasa kama Roho Mtakatifu atamfunulia huyo mtu, unajua…

Yule bibiye mdogo aliyeketi pale pale nyuma hapa kuelekea pale ninakonyooshea kidole changu, yeye anaumwa vipele vidogo vidogo. Kama wewe utaamini kwa moyo wako wote! Je, wewe unaamini hilo, bibiye, kwa moyo wako wote? Mwanamke mdogo mwenye kichwa chenye mvi aliyevaa miwani, anao, anaumwa vipele vidogo vidogo. Yeye alikuwa amesimama pale, au ameketi pale, namaanisha hivyo, akiwaza kuwa tatizo lake ni nini, akiwa anaomba moyoni mwake. Na sasa kama hilo ni sahihi, na wewe unaamini kuwa Mungu atakufanya kuwa mzima, simama juu kwa miguu yako.

Yeye aligusa nini? Nawauliza ninyi, yeye aligusa nini? Yeye yuko umbali wa yadi ishirini kutokea kwangu. Yeye alimgusa Kuhani Mkuu, na huyo Kuhani Mkuu yuko hapa! Yeye ni yule jana, leo, na hata milele na milele. Je, huoni?, Usitie shaka Hilo. Amini Hilo! Uwe na imani.

96 Sasa, singeweza kusaidia hilo, bwana. Hilo tu ni mimi-mimi naitazama tu Nuru, unaona, na Hiyo ilikwenda kutokea kwangu, na nikaiona Hiyo ikiwa imening'inia pale, na nikamwona huyo bibiye mdogo akija juu haMa mbele yangu. Naye aliendelea tu kuja mbele yangu hapa, na kuona kuwa ilikuwa ni mwanamke badala ya mwanamume, hivyo ilinipasa tu mimi kunena juu ya kile nilichokuwa nikikiona.

Ee, kama hili kanisa, kama hili kundi la watu lingeamini tu sasa hivi, na muwe tu na imani, kungetukia nini, nini ambacho kingetokea!

Bwana, sisi ni wangeni mmoja kwa mwingine. Nilitaka tu kunena na wewe, ili kwamba niweze kuwasiliana na roho yako. Hapa, wewe haupo hapa kwa ajili yako mwenyewe. Wewe upo hapa kwa ajili ya mtu fulani mwingine, huyo ni jamaa mdogo, jamaa mdogo, mvulana mdogo aliyeharibiwa katika ajali ya gari, aliyekatwakatwa vipandevipande, akachanika, vibaya mno, akiwa na hali mbaya. Wewe upo hapa, ukiwa umesimama kwa ajili yake. Hilo ni sahihi. Kama Mungu haitamsaidia huyo mvulana mdogo, itampasa yeye afe. Nifanyie hisani? Chukua hiyo leso kutoka mfukoni mwangu; nenda, iweke juu yake, katika Jina la Bwana, na usiwe na shaka. Na hebu mimi nisikie kutoka kwake, mkutano unapoendelea. Uwe na imani.

97 U hali gani, bwana? Sisi ni wageni sisi kwa sisi. Mwanamke mwingine. Je, wewe unaamini? Sasa, kumbuka, Yeye ni yule yule nje kule Yeye ambaye yuko hapa. Yeye yuko kote. Yeye yuko kila mahali.

Dada Borders, je, ni wewe uliyeketi nje kule? Siwezi kuona. Ilionekana kama kwamba ni Dada Borders akiwa ameketi pale. Mimi siwezi…Roy, mke wa Ndugu Roy Borders. Nadhani siyo. Hiyo ilikwenda moja kwa moja, ikasimama juu ya huyo bibiye. Sasa, subiri kidogo, na huenda Hiyo itakuja tena, tuone kile Hiyo ilichofanya.

Mimi ni mgeni kwako. Bwana anatufahamu sote wawili. Kama Bwana atanieleza mimi, na afanye jambo fulani hapa, kwamba wewe uko hapa kwa ajili ya nini, je, wewe utaamini kwa moyo wako wote? [Huyo dada anasema, "Ndiyo."-Mh.]

98 Bibi Borders anaendelea kusimama hapa mbele yangu, mahali fulani. Mimi…Bibi Borders yuko katika mkutano mahali fulani. [Ndugu Branham anamwambia Ndugu Roy Borders, "Je, kuna tatizo lolote na mke wako?-Mh.] Vema, hilo linaendelea tu kuja hapa. Na kuna kundi la watu, mtu fulani kando yake, na naendelea kujiuliza.

Wewe unaumwa uvimbe. Hilo ni sahihi. Je, wewe unaamini Mungu anaweza kuniambia mimi pale huo uvimbe uliko? Kwenye nyonga. Amini kwa moyo wako wote. Unayo matatizo mengi, pia, mambo mengine mengi. Amini. Hilo ni sahihi. Je, wewe unaamini kwa moyo wako wote? [Huyo dada anasema, "Ndiyo."-Mh.] Nenda, ukiamini namna hiyo, nawe uta…huo utakwisha, na Mungu atakuponya na kukufanya uwe mzima. [Huyo dada anasema, "Ndugu Branham. Huyo mwanamke alikuja pamoja na mimi, mwenye vipele vidogo vidogo, alikuja pamoja na mimi. Nami sikujua hilo hadi tulipoketi nyuma pale, yeye akasema ana vipele vidogo vidogo."] Unaona, yeye akiwa anasisimuliwa na kule kuwa katika mstari wa maombi labda hicho ndicho kilichofanya hilo, maombi ya sisi kwa sisi.

99 Hili hapa! Ee, naona! Nimemwona Bibi Borders akiwa amesimama hapa. Yeye anaomba. Na kuna mmoja-mwanamke mmoja akiwa ameketi kando na yeye pale, anayeomba, yeye ana msukumo mdogo wa damu. Kama utaamini, ukiwa umeketi papa hapa, bibiye, uamini hilo kwa moyo wako wote, na Mungu atakufanya kuwa mzima, kwa msukumo mdogo wa damu. Amina. Hilo ndilo lenyewe. Hapo ndipo maombi yalikotokea.

Kama wewe huamini mimi kuwa nabii, au, samahani, mtumishi, (hilo hukwaza watu), weka mkono wako juu ya huyo mwanamke aliyeketi kando yako, kwa sababu yeye anaumwa na mishiMa ya vena inayotanuka kupitisha damu nyingi zaidi. Unaona, hilo ni sahihi. Amina.

Amini kwa moyo wako wote sasa! Niambie wao wanagusa nini; mwanamke mdogo akiwa ameketi Male, akimwombea mwingine, hilo linaendelea tu kutokea kwenye jukwaa. Amini tu kwa moyo wako wote! Vema.

100 Njoo hapa, bibiye. Je, wewe unaamini kwa moyo wako wote? Je, unaamini? Je,

unaamini kuwa hilo tatizo la tumbo linakwenda kuMona? [Huyo dada anasema, "Ndiyo."-Mh.] Basi nenda ukale chakula chako cha usiku. Yesu Kristo anakufanya uwe mzima.

Je, wewe unaamini nini? Je, wewe unaamini Mungu anakwenda kuponya hilo tatizo la mgongo, hizo figo, na kukufanya uwe mzima? Nenda nyumbani, useme, "Yesu Kristo amenifanya mimi kuwa mzima." Uwe tu na imani, usiwe na shaka.

Njoo, bwana. Wewe ulikuwa na furaha mno ulipokuja kwenye mstari pale, namba yako ilipoitwa. Mungu huponya tatizo la moyo na anaweza kukufanya uwe mzima. Je, unaamini hilo? Basi nenda njiani mwako, ukiamini, na hilo lote litaondoka kwako, na wewe uta-wewe utafanyika kuwa mzima. Vema.

Uwe na imani. Usitie shaka. Bibiye, unawaza nini juu ya hilo? Wewe unafikiri kama mimi nikiweka mikono yangu juu yako, utakuwa mzima? Bila kusema tu chochote, niweke tu mikono yangu juu yako? [Huyo dada anasema, "Huna hata haja ya kufanya hivyo."-Mh.] Endelea. "Huna haja ya kufanya hivyo," vema, hilo ni zuri. Endelea moja kwa moja. Amina. Hiyo ndiyo njia ya kufanya hilo. Vema.

101 Njoo, bibiye. Wewe unaamini nini, dada? Je, wewe unaamini kwa moyo wako wote? Je, unajua Mungu anaweza kuniambia mimi tatizo lako ni nini, lakini wewe utaamini hilo? Basi ugonjwa wa sukari si lolote kwa Mungu, Yeye anaweza kuuponya huo. Je, unaamini hilo? Vema, endelea, uwe mzima. Amina.

Vema, bwana. Njoo, bwana. Mimi ni mgeni kwako. Kila mtu anakuambia wewe, "Jitambue mwenyewe," kwa sababu wewe una wasiwasi. Lakini huwezi kujitambua mwenyewe, kuna kitu fulani Male kinachokufanya uwe na wasiwasi. Hilo ni sahihi. Lakini umesimama mahali ulipo sasa ambapo huo umekuacha sasa. Nenda, amini hilo, na kamwe huo hautarudi tena. Nenda, amini hilo. Amina. Uwe na imani. Usitie shaka. Vema.

Mambo mengi, tatizo la bibiye, ugonjwa wa baridi yabisi. Sasa je unaamini Mungu atakufanya uwe mzima? [Huyo dada anasema, "Amina."Mh.] Nenda tu, ukisema, "Utukufu kwa Mungu," na-na uamini kwa moyo wako wote.

102 Njoo, bibiye. Je, mnaamini nje huko? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh] Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa sukari, chochote katika damu. Je, wewe huamini hilo? Hakika, Yeye anaweza. Endelea tu moja kwa moja, ukiamini, ukisema, "Amina! Bwana asifiwe!"

Je, wewe unaamini "Kuweka mikono juu ya wagonjwa, wao watapona"? Katika Jina la Bwana Yesu, nenda, uwe mzima sasa, na uamini kwa moyo wako wote.

Vema, njoo moja kwa moja, bwana. Wewe unaamini Mungu anaweza kuponya tatizo la moyo; afanye tatizo la kuzidiwa na uchovu, kila kitu, huo wasiwasi na kila kitu kiondoke kwako? Basi nenda, amini hilo katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

Je, wewe unaamini kwa moyo wako wote? Vipi juu ninyi wengine, je, mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.]

103 Viwete wenu wako wapi? Naona kiti cha magurudumu. Unasemaje, bwana? Nitazame mimi hapa. Je, wewe unaniamini mimi? Je, unaamini mimi ni mtumishi wa Mungu? Unaamini. Nitazame mimi, basi. Hilo ni, tatizo lako ni miguu yako. Unapaswa kwenda hospitalini; lakini hukuweza kufanya hilo, kwa sababu wewe uliwaza kama ungeweza kuwahi kufika hapa, ungekuwa mzima, na isingelikupasa kwenda hospitali. Hilo ni sahihi. Je, unaamini hilo? Kama ukiketi pale, wewe una hakika ya kufa; kama wenye ukoma. Daktari hawezi kukusaidia. Hivyo kwa nini usimkubali Kristo jioni hii, na kuamini hilo kwa moyo wako wote, na uinuke kutoka kwenye hicho kiti cha magurudumu, na ushike mwisho wake na ukisukume hicho huku na huku, na utoke nje mlangoni na uende nyumbani, na uwe mzima? Kwa nini usifanye hilo. Je, utaamini hilo? Basi inuka. Usitie shaka. Katika Jina la Yesu Kristo, chukua kiti chako cha magurudumu na uende nyumbani!

104 Je, wewe unaamini kwa moyo wako wote? Simama juu kwa miguu yako, mtu yeyote anayetaka kuponywa. Simama kwa miguu yako, na uamini hilo. Inuka juu! Mimi sijali ni tatizo gani ulilo nalo, ni kiwete iliyoje. Hilo halifanyi tofauti yoyote. Nakupa changamoto, inuka juu! Inuka juu, kila mtu, kila kiwete, popote ulipo. Katika Jina la Yesu Kristo, simama kwa miguu yako na uwe mzima! Ndiyo hivyo, kusanyiko lote, likiwa limesimama.

105 Sasa hebu tuinue mikono yetu kwa Mungu. Baba wa Mbinguni, Bwana, sisi tutamwona Yesu. Wewe uko hapa! Hakuna mnyonge mmoja miongoni mwetu, kila mmoja ameponywa. Tunakushukuru Wewe iliyoje, Baba! Sasa tunaomba, Mungu, kuwa Wewe utamshinda yule Mwovu katika kila tukio sasa, toa nje kila kutokuamini.

Shetani, katika Jina la Yesu, ondoka kwenye hili kusanyiko, toka nje ya haMa! Wewe umashindwa pambano. Katika Jina la bwana Yesu Kristo, wao na waponywe, kila mmoja wao.

MESSAGE hub online
www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
*"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7*